# DARAJA LA UFANISI

Elong'o PUBLISHERS

KWA WANAFUNZI WA

Kidato cha KWANZA hadi cha NNE

**KITABU CHA MASHAIRI NA SARUFI**

JACKSON NJOROGE MAINA

MARY MOTHER OF GRACE BOYS

Kimechapishwa na:

Elong'o PUBLISHERS

Published and Printed by Elong'o Publishers
P.O Box 944, Narok Kenya
Email: info@elongopublishers.co.ke
Phone: +254742433826
Website: https://elongopublishers.co.ke

© Jackson Njoroge Maina

Haki zote zimehifadhiwa. Hakuna ruhusa ya kutoa sehemu ya nakala hii au nakala nzima bila ya idhini mahususi kutoka kwa mwandishi.

Kimechapishwa mara ya kwanza 2021

ISBN: 9789914400755

# YALIYOMO

DIBAJI……………………………………………………………………………………………………………………….iv
USHAIRI
NAFSINENI………………………………………………………………………………………………………………..1
NAFSINENEWA………………………………………………………………………………………………………….1
UMBO/MUUNDO WA SHAIRI……………………………………………………………………………………..2
MISTARI MISHATA KATIKA SHAIRI……………………………………………………………………………..4
UHURU WA MSHAIRI/IDHINI ZA KISHAIRI…………………………………………………………………..5
LUGHA NATHARI………………………………………………………………………………………………………..7
AINA ZA MASHAIRI……………………………………………………………………………………………………..8
BAHARI ZA USHAIRI…………………………………………………………………………………………………..11
MAUDHUI KATIKA MASHAIRI……………………………………………………………………………………..17
DHAMIRA…………………………………………………………………………………………………………………..18
TAKRIRI/ URUDIAJI……………………………………………………………………………………………………..18
TASWIRA……………………………………………………………………………………………………………………..20
TONI KATIKA SHAIRI…………………………………………………………………………………………………..21
MBINU ZA KIMTINDO KATIKA MASHAIRI……………………………………………………………………..22
MAANA YA KITAMATHALI NA MAANA YA KIJUUJUU KATIKA USHAIRI……………………………..24
SARUFI
SAUTI…………………………………………………………………………………………………………………….. 26
VIJALIZO……………………………………………………………………………………………………………………..33
VITATE NA VISAWE……………………………………………………………………………………………………..33
NYAKATI NA HALI………………………………………………………………………………………………………..34
NGELI…………………………………………………………………………………………………………………………..36
UMOJA NA WINGI……………………………………………………………………………………………………….42
HALI YA KUKANUSHA……………………………………………………………………………………………………43
HALI YA KUYAKINISHA………………………………………………………………………………………………….45
UAKIFISHAJI………………………………………………………………………………………………………………….46
UDOGO, WASTANI NA UKUBWA……………………………………………………………………………………52
NOMINO………………………………………………………………………………………………………………………55
VIHUSISHI…………………………………………………………………………………………………………………….58
VITENZI………………………………………………………………………………………………………………………..59
VIVUMISHI……………………………………………………………………………………………………………………62
VIWAKILISHI…………………………………………………………………………………………………………………68
VIELEZI…………………………………………………………………………………………………………………………71
VIHISISHI………………………………………………………………………………………………………………………74
KIIMA NA KIARIFA………………………………………………………………………………………………………..76
SHAMIRISHO/ YAMBWA NA CHAGIZO…………………………………………………………………………..77

**AINA ZA SENTENSI……………………………………………………………………………………………………...80**
**VISHAZI…………………………………………………………………………………………...........................82**
**VIRAI………………………………………………………………………………………………………………………...85**
**MWINGILIANO WA MANENO………………………………………………………………………………………88**
**VIUNGANISHI……………………………………………………………………………………………………………91**
**SENTENSI TATA…………………………………………………………………………………………………………93**
**VIREJESHI…………………………………………………………………………………………………………………95**
**MATUMIZI YA VIAMBISHI MBALIMBALI…………………………………………………………………….97**
**A UNGANIFU…………………………………………………………………………………………………………….104**
**UCHANGANUZI WA SENTENSI………………………………………………………………………………...105**
**USEMI HALISI NA USEMI WA TAARIFA……………………………………………………………………..113**
**VIAMBISHI NA MOFIMU………………………………………………………………………………………….116**
**MNYAMBULIKO WA VITENZI…………………………………………………………………………………..122**
**UUNDAJI WA MANENO…………………………………………………………………………………………..124**
**VINYUME VYA VITENZI…………………………………………………………………………………………..126**
**MIUNDO YA SENTENSI……………………………………………………………………………………………127**

# DIBAJI

Kitabu hiki kimeandikwa ili kiwaauni wanafunzi katika vipengee tata vya sarufi na mashairi. Mada mbalimbali za sarufi na mashairi zimejadiliwa kwa namna iliyo rahisi kwa mwanafunzi kuelewa. Natoa shukrani zangu za dhati kwa wote waliofanikisha maandalizi ya kazi hii.

# USHAIRI

## NAFSINENI

Ni yule mtu au watu wanaowasilisha ujumbe katika shairi. Baadhi ya vielekezi vitakavyomsaidia mwanafunzi kubainisha nafsineni katika shairi ni kuchunguza ni nani anayetoa ujumbe au kuchunguza maneno yanayoonyesha ujumbe unatoka kwa nani.

**Mfano**

Tujikakamue waja, tuuondoe utawala dhalimu.

Nafsineni ni **mwanamapinduzi**. Anawahimiza watu wauondoe utawala dhalimu.

Ninawasihi wananchi, mnikabidhi uongozi.

Nafsineni ni **mwanasiasa** anayewarai wananchi wampe nafasi ya kuongoza.

Maisha yana ngambi nyingi

Tutathmini

Tujitolee

Tusikate tamaa

Tukaze kamba

Tutashinda

Nafsineni ni **mshauri**. Anatoa ushauri kwa waja watie bidii na wajitolee kwani watayashinda matatizo yote.

## NAFSINENEWA

Ni wale ambao ujumbe unawasilishwa kwao. Nafsineni huwasilisha ujumbe kwa nafsinenewa.

**Mfano**

Tujikakamue waja, tuuondoe utawala dhalimu.

Nafsinenewa ni **wananchi**. Wanahimizwa wauondoe kabisa utawala dhalimu.

Tuepuke kila dhambi, tusilie jahanamu.

Nafsinenewa ni **waumini**. Wanahimizwa waepuke dhambi ili wasi-lie jahanamu.

## UMBO/MUUNDO WA SHAIRI

Ili kueleza muundo wa shairi, mwanafunzi anafaa kuzingatia mambo yafuatayo:

(a) aeleze idadi ya beti katika shairi.

(b) kuonyesha idadi ya mistari katika ubeti.

(c) kufafanua kuhusu vipande katika mistari.

(d) kudhihirisha mpangilio wa vina katika shairi.

(e) kutoa maelezo ikiwa shairi lina kibwagizo au kiishio.

(f) kueleza kuhusu idadi ya mizani katika shairi.

**Mfano**

Eleza **muundo** katika shairi hili.

Maisha yana ngambi nyingi
Tutathmini
Tujitolee
Tusikate tamaa
Tukaze kamba
Tutashinda.

Dhiki humkabili binadamu
Masaibu humkusa mja
Ila
stahamala,
bidii na
ukakamavu
humpa mafanikio makubwa.

**Muundo wa shairi hili**

(a) Shairi hili lina beti mbili.

(b) Idadi ya mistari inatofautiana kutoka ubeti mmoja hadi mwingine. Ubeti wa kwanza una **mistari 6** ilhali ubeti wa pili una **mistari saba**.

(c) Shairi lenyewe halina vipande. Mfano, mstari wa pili katika ubeti wa pili ambao ni **Masaibu humkusa mja** hauna vipande.

(d) Halina urari wa vina. Mpangilio wa vina katika ubeti wa kwanza ni:

____________ngi

____________ni

____________e

____________a

____________mba

____________nda

(e) Shairi halina kibwagizo. Mstari wa mwisho katika ubeti wa kwanza ni **Tutashinda** ilhali mstari wa mwisho katika ubeti wa pili ni **Humpa mafanikio makubwa**.

(f) Idadi ya mizani inatofautiana kutoka mstari mmoja hadi mwingine.

Mstari wa kwanza katika ubeti wa kwanza una **mizani 9**. Mstari wa tatu katika ubeti wa kwanza una **mizani 5**.

Katika hali nyingine mwanafunzi anaweza akahitajika kueleza muundo wa ubeti mmoja wa shairi.

**Mfano**

Nawapa mimi nasaha, ndugu zangu waumini,

Tuepuke kila karaha, dhambi za maabadini,

Ombeni Mola msamaha, adhabu tuepukeni,

Sisi waja wakosefu, tuwe wenye shukurani.

**Muundo wa ubeti huu**

(a) Ubeti huu una mistari minne.

(b) Kila mstari una vipande viwili. Mfano mstari wa pili una vipande

viwili, ukwapi na utao.

Tuepuke la karaha, dhambi za maabadini

ukwapi utao

(c) Kila mstari una mizani minane.

(d) Mpangilio wa vina ni:

______ ha ________ ni

______ ha ________ ni

______ ha ________ ni

______ fu ________ ni

## MISTARI MISHATA KATIKA MASHAIRI

Hii ni mistari katika shairi ambayo haijakamilika kimaana. Hukamilishwa kimaana na mistari inayofuata.

**Tazama ubeti ufuatao:**

Dhiki humkabili binadamu.

Masaibu humkusa mja.

Ila

stahamala

bidii na

ukakamavu

humpa mafanikio makubwa.

Mstari wa tano wa ubeti huu ambao ni **bidii na** ni mstari mshata. Haujakamilika kimaana. Unakamilishwa kimaana na mstari unaofuata ambao ni **ukakamavu**.

Ili kubainisha mistari mishata ni muhimu kuchunguza mistari ili kuitambua ile ambayo maana yake haijakamilika.

**Mfano wa pili**

Yaliyo mwangu mtimani

Ni mengi na yanakera

Usiku yananihini usingizi

Na mchana yananipa maumivu

Nabaki katika

njia panda

Niyafichue au nizidi kuyabania.

Mstari wa tano, **Nabaki katika** ni mstari mshata. Unakamilishwa kimaana na mstari unaofuata ambao ni **njia panda**.

## UHURU WA MSHAIRI/IDHINI ZA KISHAIRI

Ni njia ambazo mtunzi wa shairi anazitumia **ili kutosheleza mahitaji ya kiarudhi**.

Uhuru wa mshairi hushirikisha:

### (a) Kuboronga sarufi/ kufinyanga sarufi

Kuboronga sarufi ni kutozingatia mpangilio sahihi wa maneno katika mishororo.

Mshairi huutumia uhuru huu ili kuleta **urari wa vina** na **mahadhi ya kimuziki**.

**Mfano**

Yaliyo mwangu mtimani

Ni mengi na yanakera

Usiku yananihini usingizi

Katika mstari wa kwanza, kuna kuboronga sarufi **yaliyo mwangu mtimani**. Mshororo huu unafaa kuwa **yaliyo mtimani mwangu**.

### (b) Inkisari

Ni uhuru wa kufupisha maneno katika shairi. Madhumuni hasa ya kufupisha maneno ni kuleta **urari wa mizani** katika shairi.

**Mfano**

Walodai ni tamaa, ya waja ilokithiri.

Katika mstari huu neno **walodai** limefupishwa, linafaa kuwa **waliodai**. Mshairi ametumia uhuru huu ili kuleta urari wa mizani.

Vilevile neno **ilokithiri** limefupishwa. Linafaa kuwa **iliyokithiri**.

### (c) Mazida

Ni kurefusha maneno ili kuleta urari wa mizani.

**Mfano**

Za kulevya mashuleni, jijini na vijijini,

Wanainchi hatarini, taabu kote nchini,

Ni muhali kunawini, uchumi kubaki chini,

Viongozi tupigane, tulikabili janga hili.

Neno **wanainchi** katika mstari wa pili limerefushwa. Linafaa kuwa **wananchi**.

Mshairi ametumia uhuru huu ili kuleta urari wa mizani.

### (d) Tabdila

Ni kubadilisha silabi ya mwisho katika neno ili kuleta urari wa vina. Uhuru huu hutumika mwishoni mwa vipande katika mistari.

**Mfano**

Za kulevya mashuleni, jijini na vijijini

Wananchi hatarini, taabu kote nchini

Ni muhali kunawini, uchumi kubaki chini

Viongozi tupigane tukabili janga hili

Kuna matumizi ya tabdila katika neno **kunawini** katika mstari wa tatu. Silabi ya mwisho **ni** imetumika badala ya **ri**. Neno lenyewe linafaa kuwa kunawiri.

Uhuru huu umetumika ili kuleta urari wa vina katika shairi.

### (e) Maneno ya kilahaja

Mtunzi anaweza akatumia maneno katika shairi ambayo yanatoka katika lahaja mbalimbali za Kiswahili.

**Mfano**

Alisimama kando ya ndiya

Mawazo mzomzo akilini

Wananti walimzomea

Afanya lipi aache lipi?

Maneno **ndiya** na **wananti** ni ya kilahaja. Yanafaa kuwa **njia** na **wananchi**.

### (f) <u>Utohozi</u>

Ni kuyachukua maneno ya lugha nyingine na kuyafanya yawe na muundo sawa na maneno katika lugha ya Kiswahili.

Limetokea janga hili, binadamu wateseka

Ugonjwa hatari nduli, waangamiza hakika

Wataalamu wanakili, wao pia watishika

Wapendwa tuvae maski, tujikinge na maradhi.

Neno **maski** limetoholewa. Linatokana na neno "**mask**" la Kiingereza.

### (g) <u>LUGHA NATHARI</u>

Lugha nathari katika shairi pia hujulikana kama **lugha ya kiriwaya**, **lugha tutumbi**, **lugha ya mjazo** au **ya mwendelezo**. Mtunzi wa mashairi aghalabu hutumia lugha ya mkato katika kuwasilisha ujumbe wake. Mwanafunzi anapoandika ubeti wa shairi kwa lugha nathari, anafaa auandike ubeti huo kwa lugha ya kawaida.

**Mambo ya kuzingatia unapoandika ubeti wa shairi kwa lugha nathari.**

(a) Kusoma ubeti unaohitajika kueleza kwa lugha ya nathari na kuelewa maana yake na kisha kuuandika kwa lugha ya kawaida bila kupotosha maana.

(b) Ubeti unaohusika ugeuzwe na kuwa aya moja.

(c) Lugha sanifu itumike. Ikiwa kuna maneno yaliyofupishwa au kurefushwa, maneno hayo yaendelezwe kwa njia sahihi.

(d) Unaweza ukaongeza maneno katika ubeti wa shairi. Hata hivyo, maneno yaliongezwa yasipotoshe ujumbe katika ubeti unaohusika.

**Mfano ubeti wa 1**

Nawapa mimi nasaha, ndugu zangu waumini

Tuepuke la karaha, dhambi za maabadini

Sali Mola msamaha, adhabu tuepukeni

Sisi waja wakosefu, tuwe wenye shukurani.

**Kwa lugha nathari**

Mshairi anasema kuwa anawapa wao ushauri ambao ni ndugu zake walio waumini. Anawaambia kwamba waepuke mambo yaliyo ya karaha na dhambi ambazo ni za mahali pa kuabudu. Anawahimiza watu waombe msamaha kutoka kwa Mungu ili waepuke adhabu kutoka kwa Mungu. Anasema kuwa sisi ni waja ambao tumekosea na tunafaa tuwe na shukrani.

**Mfano ubeti wa 2**

Dhiki humkabili binadamu

Masaibu humkusa mja

Ila

stahamala

bidii na

ukakamavu

Humpa mafanikio makubwa.

**Kwa lugha nathari**

Mshairi anasema kwamba matatizo huweza kumkabili binadamu. Matatizo pia humtokea binadamu, lakini ikiwa atakuwa na stahamala bidii na ukakamavu, basi atapata mafanikio makubwa.

## AINA ZA MASHAIRI

Kuna aina mbili kuu za mashairi.

### (a) MASHAIRI HURU/MASHAIRI YA KIMAPINDUZI

Haya ni mashairi ambayo hutungwa bila ya mshairi kufungwa na sheria au kanuni za kutunga mashairi. Mtunzi anaweza kuwasilisha ujumbe wake bila ya kufuata arudhi za utunzi.

Mtunzi wa mashairi ambayo ni huru anaweza akatunga shairi ambalo:

(a) halina urari wa vina.

(b) halina urari wa mizani.

(c) idadi ya mistari inatofautiana kutoka ubeti mmoja hadi mwingine.

(d) halina vipande.

(e) mstari wa mwisho unabadilikabadilika.

**Mfano wa shairi huru**

Maisha yana ngambi nyingi
Tutathmini
Tujitolee
Tusikate tamaa
Tukaze kamba
Tutashinda.

Dhiki humkabili binadamu
Masaibu humkusa mja
Ila
stahamala
bidii na
ukakamavu
Humpa mafanikio makubwa.

Hili ni shairi la aina gani? Thibitisha.

Ni **shairi huru**. Hii ni kwa sababu :

(a) Halina urari wa vina. Vina mwishoni mwa mstari vinabadilika-badilika. Mpangilio wa vina katika ubeti wa kwanza ni:

____________ngi

____________ni

____________e

____________a

____________mba

____________nda

(b) Halina urari wa mizani. Mstari wa tano katika ubeti wa kwanza una **mizani mitano** ilhali mstari wa kwanza katika ubeti wa kwanza una **mizani tisa**.

(c) Idadi ya mistari inatofautiana kutoka ubeti mmoja hadi mwingine. Ubeti wa kwanza una mistari sita ilhali ubeti wa pili una mistari saba.

(d) Shairi lenyewe halina vipande. Mstari wa kwanza katika ubeti wa pili ambao ni **Dhiki humkabili binadamu** hauna vipande.

(e) Shairi hili halina kibwagizo. Mstari wa mwisho katika ubeti wa kwanza ni **Tutashinda** ilhali mstari wa mwisho katika ubeti wa pili ni **Humpa mafanikio makubwa**.

### (b) AINA YA SHAIRI KWA KUZINGATIA IDADI YA MISTARI KATIKA UBETI

Aina ya pili ya shairi hutegemea idadi ya mistari katika ubeti. Ikiwa shairi lina mistari minne katika kila ubeti litakuwa ni la aina ya **tarbia**.

Mistari mitano ni **takhimisa**.

Mistari sita ni **tasdisa**.

Mistari miwili ni **tathnia.**

Mistari mitatu ni **tathlitha.**

Mistari saba ni **usaba**.

**Mfano**

Nawapa mimi nasaha, ndugu zangu waumini

Tuepuke la karaha, dhambi za maabadini

Sali Mola msamaha, adhabu tuepukeni

Sisi waja wakosefu, tuwe wenye shukurani.

Ewe Mola na Jalali, tuongoze maishani

Tupe nguvu pia hali, tushike neno moyoni

Tuwapo kwenye kitali, itawale nyingi imani

Sisi waja wakosefu, tuwe wenye shukurani .

Bainisha shairi lililo hapo juu.

Hili ni shairi la **tarbia**. Hii ni kwa sababu lina mistari minne katika kila ubeti.

## BAHARI ZA USHAIRI

Mashairi huwekwa katika bahari mbalimbali kwa kutegemea vigezo kama mizani, mpangilio wa vina, idadi ya vipande katika mstari, namna maneno yanavyojitokeza katika mistari katika shairi, au jumla ya bahari zinazodhihirika katika shairi.

### (a) Mathnawi

Hili ni shairi ambalo lina vipande viwili katika kila mstari.

Kipande cha kwanza cha ushairi hujulikana kama **ukwapi** na cha pili **utao**.

Za kulevya mashuleni, jijini na vijijini

Wanainchi hatarini, taabu kote nchini

Ni muhali kunawini, uchumi kubaki chini

Viongozi tupigane, tukabili janga hili.

Eleza shairi lililo hapo juu kwa kuzingatia vipande.

Hili ni shairi la **mathnawi** kwa kuwa kila mstari una vipande viwili, ukwapi na utao.

Mstari wa kwanza, **za kulevya mashuleni, jijini na vijijini,** una vipande viwili.

Kipande cha kwanza(ukwapi) ni **za kulevya mashuleni** ilhali kipande cha pili (utao) ni **jijini na vijijini**.

### (b) Ukawafi

Hili ni shairi lililo na vipande vitatu katika kila mstari.

**Mfano**

Siafu ni hatari, wanapoteseka, huungana

Mikono hushikana, huapa, kupinga madhila

Ari huwajaa, nafsini, na roho za dhaifu

Wana ghadhabu, masaibu, yawakaba koo.

Ainisha shairi lililo hapo juu kwa kuzingatia vipande.

Ni la **ukawafi**. Hii ni kwa sababu lina vipande vitatu katika kila mstari. Mstari wa mwisho una vipande vitatu.

Wana ghadhabu, masaibu, yawakaba koo

ukwapi utao mwandamizi

### (c) Mavue

Ni shairi lililo na vipande vinne katika kila mshororo.

Alijuta, akajilaumu, moyoni, na akilini

Kapita, kahujumu, wanyonge, masikini

Furuta, maadamu, ana nguvu, uongozini

Seneta, dhalimu, kajitia, kamba shingoni.

Ainisha shairi hili kwa kuzingatia vipande.

Ni la **mavue**. Hii ni kwa sababu lina vipande vinne katika kila mstari.

**Mfano**, mstari wa pili wa ubeti huo una vipande vinne.

Kapita, kahujumu, wanyonge, maskini

ukwapi utao mwandamizi ukingo

### (d) Msuko

Hili ni shairi ambalo mstari wake wa mwisho ni mfupi. Idadi ya mizani katika mstari wa mwisho ni michache ikilinganishwa na mistari mingine.

**Mfano,**

Naandika vitabuni, ili mpate kujua

Mfahamu kwa mapani, msije mkajutia

Mewaponza maishani, moyoni ilowajaa

Tamaa hasara.

Ainisha shairi lililo hapo juu kwa kuzingatia mizani.

Ni la **msuko**. Hii ni kwa sababu mstari wa mwisho ni mfupi. Mstari wa mwisho una **mizani sita**. Mistari hiyo mingine ina mizani kumi na sita.

**(e) Ukara**

Ni shairi ambalo vina vya mgao mmoja vinabadilika kutoka ubeti mmoja hadi mwingine na vina vya mgao mwingine havibadiliki kutokea ubeti wa kwanza hadi ubeti wa mwisho. Tazama shairi lifuatalo.

Nawapa mimi nasa**ha**, ndugu zangu waumi**ni**

Tuepuke la kara**ha**, dhambi za maabadi**ni**

Sali Mola msama**ha**, adhabu tuepuke**ni**

Sali waja wakose**fu**, tuwe wenye shukura**ni**.

Ewe Mola na Jala**li**, tuongoze maisha**ni**

Tupe nguvu pia ha**li**, tushike neno moyo**ni**

Tuwapo kwenye kita**li**, tawale nyingi ima**ni**

Sisi waja wakose**fu**, tuwe wenye shukura**ni.**

Ainisha shairi hili kwa kuzingatia mpangilio wa vina.

Hili ni shairi la **ukara**. Hii ni kwa sababu kina cha mwisho hakibadiliki. Kina hicho ni **ni**. Vina vya ndani hata hivyo vinabadilika kutoka ubeti hadi mwingine. Kina cha kati katika mistari ya kwanza mitatu katika ubeti wa kwanza ni **ha**. Kina cha kati katika mistari ya kwanza mitatu katika ubeti wa pili ni **li**.

**(f) Mtiririko**

Mashairi katika bahari ya mtiririko huwa na vina vya ndani vinavyo-fanana katika beti zote na vina vya mwisho hufanana katika beti zote.

Naandika vitabu**ni**, ili mpate kuju**a**

Mfahamu kwa mapa**ni**, msije mkajuti**a**

Mewaponza maisha**ni**, moyoni ilowaja**a**

Tamaa hasara.

Viongozi wamebu**ni**, nyingi hila na nji**a**

Wahodhi nyingi pau**ni**, halali yake rai**a**

Wananchi wafanye ni**ni**, waondokee udhi**a**

Tamaa hasara.

Ainisha shairi hili kwa kuzingatia mpangilio wa vina.

Ni shairi la **mtiririko**. Hii ni kwa sababu kina cha kati ambacho ni **ni** katika mistari ya kwanza mitatu katika beti zote hakibadiliki. Aidha kina cha mwisho katika mistari ya kwanza mitatu katika beti zote ambacho ni **a** hakibadiliki. Kina cha ndani hakibadiliki isipokuwa katika mstari wa mwisho. Hali kadhalika kina cha mwisho hakibadiliki isipokuwa katika mstari wa mwisho.

### (g) Ukaraguni

Ni shairi ambalo vina vya ndani na vya nje vinalingana katika kila ubeti lakini vinabadilika kutoka ubeti mmoja hadi mwingine.

**Mfano**

Limetokea janga hi**li**, binadamu wateseka**ka**

Ugonjwa hatari ndu**li**, waangamiza haki**ka**

Wataalamu wanaki**li**, wao pia watishi**ka**

Wapendwa tuvae ma**ski**, tujikinge na mara**dhi**.

Mewasibu wengi wa**tu**, wakubwa pia wado**go**

Furifuri zahana**ti**, taabika si kido**go**

Matabibu wenye vye**ti**, wote wamepata pi**go**

Wapendwa tuvae ma**ski**, tujikinge na mara**dhi**.

Ainisha shairi hili kwa kuzingatia mpangilio wa vina.

Ni la bahari ya **ukaraguni**. Hii ni kwa sababu vina vya kati na vile vya

nje katika mistari ya kwanza mitatu vinafanana lakini vinatofautiana kutoka ubeti mmoja hadi mwingine.

**(h) Pindu**

Ni shairi ambalo hutumia neno la mwisho katika kila mgao au mstari kuwa neno kwanza katika mgao au mstari unaofuata.

**Mfano 1**

Walimwengu wote **walia**, **walia** utu wadai

Wadai **waangamia**, **waangamia** felia

Felia na **fidhulia, fidhulia** na datia

Utu umeadimika, kama mizizi ya mawe.

**Mfano wa 2**

Utashi wa binadamu, hufaa **aushini**

**Aushini** takadamu, tajirika **maishani**

**Maishani** kazuumu, akaridhika moyoni

Nyingi jaha anudhumu, kajitenga nukusani.

**(i) Kikwamba**

Ni shairi ambalo lina maneno ambayo yanarudiwa mwishoni mwa kila mstari au mwanzoni mwa kila mstari.

**Mifano**

**Mfano wa kwanza**

**Mapenzi** ni kitu aula, huliwaza na kupoza

**Mapenzi** hayana hila, la mja aliyegaza

**Mapenzi** hayana dhila, wapenzi kipatiliza

**Mapenzi** ni almasi, yafariji yaongoa.

**Mfano wa pili**

Haulipi **uovu**

Unakera **uovu**

Tamaa ni **uovu**

Wivu ni **uovu**

Uovu uovu

Ainisha shairi hili la pili kwa kuzingatia maneno.

Ni shairi la **kikwamba** kwa kuwa neno **uovu** linarudiwa mwishoni mwa kila mstari.

**(j) <u>Sakarani</u>**

Haya ni mashairi ambayo yamechanganya bahari mbalimbali.

Naandika vitabuni, ili mpate kujua

Mfahamu kwa mapani, msije mkajutia

Mewaponza maishani, moyoni ilowajaa

Tamaa hasara.

Viongozi wamebuni, nyingi hila na njia

Wahodhi nyingi pauni, halali yake raia

Wananchi wafanye nini, waondokee udhia

Tamaa hasara.

Shairi hili ni la bahari ya **sakarani**. Hii ni kwa sababu limechanganya bahari mbalimbali

Ni **msuko** kwa kuwa kibwagizo chake ni kifupi. Mstari wa mwisho una mizani sita ilhali mistari hiyo mingine ina mizani kumi na sita. Ni la **mtiririko** kwa kuwa kina cha kati ni **ni** katika mistari ya kwanza mitatu. Kina cha mwisho ni **a** katika mistari ya kwanza mitatu katika kila ubeti. Ni la bahari ya **mathnawi** kwa kuwa mistari ya kwanza mitatu ina vipande viwili katika kila mshororo.

**Mfano,** ubeti wa kwanza, mstari wa kwanza

<u>Naandika vitabuni</u>, <u>ili mpate kujua</u>

ukwapi utao

**(k) <u>Kikai</u>**

Ni shairi ambalo lina kipande kimoja kifupi katika mstari ukilinganisha

na kipande hicho kingine. Mgao mmoja katika mstari huwa na mizani michache.

**Mfano**

Kimtazama machoni, sawijika

Wasiwasi tamakani, kahizika

Unafiki wamuhini, mefichuka

Mzandiki mbuya

Utao una mizani minne hali ukwapi una mizani minane.

**(l) <u>Mandhuma</u>**

Ni shairi ambalo upande mmoja wa mstari katika shairi hutoa hoja au swali na upande mwingine hutoa jibu au ufafanuzi katika mstari uo huo.

**Mfano**

Masaibu ya wanyonge, yana mwisho

Ukweli ukidhihiri, uongo hujitenga

Viongozi makatili, huwaponza wananchi.

**(m) <u>Ngonjera</u>**

Haya ni mashairi yanayoshirikisha watu wawili au vikundi viwili vya watu ambavyo vinajibizana kutegemea upande wanaounga mkono katika mada fulani. Ubeti wa mwisho katika mashairi haya huonyesha maafikiano baina ya watu au makundi ya watu waliokuwa wanajibizana.

**<u>MAUDHUI KATIKA MASHAIRI</u>**

Ni mawazo, masuala au ujumbe ambao unawasilishwa na mtunzi wa shairi. Mwanafunzi anaweza kutambua maudhui ikiwa atalisoma shairi kwa makini. Upo uwezekano wa mtunzi wa shairi kuwasilisha maudhui mbalimbali. Ni wajibu wa mwanafunzi kulisoma shairi na kuyatambua maudhui yote yanayojitokeza katika shairi.

Za kulevya mashuleni, jijini na vijijini

Wanainchi hatarini, taabu kote nchini

Ni muhali kunawini, uchumi kubaki chini

Viongozi tupigane, tukabili janga hili.

Eleza ujumbe katika ubeti wa shairi hili.

Maudhui katika shairi hili ni kuhusu **dawa za kulevya**. Katika mstari wa pili, mshairi anasema kwamba wananchi wapo hatarini kutokana na dawa za kulevya. Katika mstari wa tatu anasema kwamba ni vigumu kwa taifa kunawiri ikiwa kuna matumizi ya mihadarati nchini.

## DHAMIRA

Ni lengo au madhumuni ya mtunzi wa shairi. Lengo la mshairi linaweza likawa ni kusifu, kuelimisha, kusihi, kuonya, kuzindua, kuhimiza, kukashifu, kutahadharisha kupongeza au kusuta.

Limetokea janga hili, binadamu wateseka

Ugonjwa hatari nduli, waangamiza hakika

Wataalamu wanakili, wao pia watishika

Wapendwa tuvae maski, tujikinge na maradhi

Dhamira ya mtunzi ni **kuwaonya watu kuhusu athari za ugonjwa hatari uliotokea**. Anasema katika mstari wa pili kwamba ugonjwa huu ni hatari na unaangamiza. Dhamira nyingine ya mtunzi ilikuwa ni **kuwahimiza watu kuvaa maski** ili waepuke ugonjwa hatari uliotokea. Katika mstari wa mwisho anasema kwamba tuvae maski ili tusipatwe na huu ugonjwa hatari.

## TAKRIRI/URUDIAJI

Ni uruduaji wa sauti, silabi, neno au kifungu cha maneno katika shairi. Takriri hutumika ili:

(a) kusisitiza ujumbe ambao unawasilishwa.

(b) kuleta mahadhi ya kimuziki katika shairi.

(c) kulifanya shairi kuwa rahisi kulikariri.

## AINA ZA TAKRIRI

(I)Urudiaji wa mshororo. Ikiwa mstari wa mwisho wa shairi umerudiwa (kibwagizo), basi tunasema kuna takriri ya mshororo.

**Mfano**

Limetokea janga hili, binadamu wateseka
Ugonjwa hatari nduli, waangamiza hakika
Wataalamu wanakili, wao pia watishika
**Wapendwa tuvae maski, tujikinge na maradhi**.

Mewasibu wengi watu, wakubwa pia wadogo
Furifuri zahanati, taabika si kidogo
Matabibu wenye vyeti, wote wamepata pigo
**Wapendwa tuvae maski, tujikinge na maradhi**.

Katika shairi hili kuna urudiaji wa mstari. Mstari wa mwisho

katika shairi ambao ni **wapendwa tuvae maski, tujikinge na maradhi** umerudiwa katika beti zote.

### (ii) Urudiaji wa neno

Neno moja hurudiwa katika shairi.

**Mfano**

Haulipi **uovu**
Unakera **uovu**
Tamaa ni **uovu**
Wivu ni **uovu**
**Uovu uovu**

### (iii) Urudiaji wa virai (kifungu cha maneno)

Uradidi huu hushirikisha kifungu cha maneno kikijitokeza katika sehemu fulani ya shairi.

**Mfano**

**Mapenzi hayana** hila, la mja aliyegaza
**Mapenzi hayana** dhila, mapenzi kipatiliza

Kuna urudiaji wa kirai **mapenzi hayana** katika mistari hiyo miwili.

### (iv) Urudiaji wa silabi

Katika aina hii ya urudiaji, silabi moja hurudiwarudiwa.

**Mfano**

**Kiki**liza **ki**mponze, **ki**na doa takilifu

Katika mstari huu, kuna urudiaji wa silabi **ki**.

## TASWIRA

Taswira ni maelezo ambayo hujenga picha kwenye akili ya msomaji.

## AINA ZA TASWIRA

### (a) Taswira uoni (muono)

Ni aina ya taswira inayotokana na maelezo yanayotufanya tuone hali inayochorwa.

**Mfano**

Mavazi yake mekundu yalikuwa yamechakaa.

Hapa tunapata taswira muono ya mavazi mekundu na yaliyochakaa.

### (b) Taswira muonjo

Ni taswira inayotokana na kupata ladha ya vyakula au vinywaji vinavyoliwa.

Alikula chakula kilichokolea chumvi.

Kuna taswira ya chakula kilichotiwa chumvi kiasi za kuridhisha.

### (c) Taswira sikivu

Hutokana na sauti ya vitu tunayoisikia.

Alipokuwa amelala, alisikia mbisho hafifu uliofuatiwa na sauti iliyoashiria maumivu.

Kuna taswira sikivu inayodhihirika ya mtu anayebisha na mtu aliye na maumivu.

### (d) <u>Taswira mnuso</u>

Ni maelezo yanayotolewa yanayomfanya msomaji kuhisi harufu ya kitu fulani.

**Mfano**

Mtaani harufu nzuri ya vibanzi vilivyokuwa vinapikwa ilihanikiza.

Taswira inayochorwa hapa ni taswira mnuso ya harufu nzuri ya vibanzi.

### (e) <u>Taswira mguso</u>

Ni aina ya taswira inayotokana na vitu tunavyovishika au kuvigusa.

**Mfano**

Alipoingia katika chumba kilichokuwa na giza, mikono yake ilipapasa ukuta uliokuwa laini hadi alipoifikia swichi na akaiwasha.

Taswira mguso inadhihirika wakati inaposemekana alipapasa ukuta uliokuwa laini hadi alipoifikia swichi.

## <u>TONI KATIKA SHAIRI</u>

Toni katika shairi hutokana na hisia ambazo anazifungamanisha mtunzi katika kuuwasilisha ujumbe wake. Toni inaweza ikawa ya huzuni, mapenzi, kuzindua, kusifu, kukashifu, furaha miongoni mwa toni nyinginezo.

**Mfano**

Limetokea janga hili, binadamu wateseka

Ugonjwa hatari nduli, waangamiza hakika

Wataalamu wanakili, wao pia watishika

Wapendwa tuvae maski, tujikinge na maradhi.

Toni katika shairi hili ni ya **huzuni**. Hii ni kwa sababu kuna ugonjwa uliozuka na unawafanya binadamu kuteseka. Ugonjwa huu unaangamiza na wataalamu wametishika.

## MBINU ZA KIMTINDO KATIKA MASHAIRI

Baadhi ya mbinu za kimtindo zinazotahiniwa mara kwa mara ni:

**(a) Kinaya**

Kinaya ni kinyume cha matarajio.

**Mfano**

Umaskini uliompa furaha

Ni kinaya kwamba umaskini unampa furaha.

**(b) Tasfida/Tauria**

Ni kutumia maneno ya adabu ambayo hayazui hisia ikiwa yatatamkwa waziwazi.

**Mfano**

Alienda kutawabali. (badala ya kutumia neno linaloonyesha kwenda haja ndogo)

**(c) Tanakuzi**

Ni mbinu ya kusisitiza jambo kwa kutumia maneno yanayokinzana.

**Mfano**

Alitokwa na machozi ya furaha.

Alilia na kucheka.

Kitendo cha kulia na wakati uo huo kucheka ni tanakuzi.

**(d) Chuku**

Ni kutilia chumvi jambo fulani kwa madhumuni ya kusisitiza.

**Mfano**

Machozi yalimtiririka na kufanya mto mkubwa. Machozi kufanya mto mkubwa ni chuku.

**(e) Usambamba**

Ni urudiaji wa sauti, maneno au vifungu fulani vya maneno katika mistari katika shairi.

**Mifano**

**Mfano wa 1**

Kikiliza kimponze, kina doa takilifu. Katika mstari huu, sauti ki imerudiwa.

**Mfano 2**

**Tamaa hatari, tamaa huhasiri, tamaa huponza**. Katika mstari huu neno tamaa limerudiwa katika mstari.

Urudiaji huu unafahamika kama usambamba.

**(f) Sitiari**

Ni ulinganishi wa moja kwa moja bila kutumia maneno ya kulinganisha.

**Mfano**

Tamaa ni sumu.

Tamaa inalinganishwa na sumu.

**(g) Tashhisi**

Ni kuvipa vitu visivyokua na uhai sifa za kitu chenye uhai.

**Mfano**

Tamaa ilimchekelea.

Tamaa inapewa uwezo wa mwanadamu wa kucheka.

**(h) Tashbiha**

Ni usemi wa kulinganisha kitu kimoja na kingine kwa kutumia maneno ya kulinganisha kama mithili ya, sawasawa na, kama na ja.

**Mfano**

Mapenzi ja sukari.

Mapenzi yanalinganishwa na sukari.

**(i) Nahau**

Ni kifungu cha maneno ambacho huwasilisha maana tofauti na maana iliyo katika maneno hayo.

**Mfano**

laza damu

Hii ni nahau yenye maana ya kuzembea.

### (j) <u>Usimulizi</u>

Usimulizi katika ushairi ni hali ambapo mtunzi wa shairi huliwasilisha shairi lake kwa mtindo wa kutamba au kusimulia kama hadithi.

### (k) <u>Maswali ya balagha</u>

Haya ni maswali ambayo hayahitaji majibu. Maswali haya hutumiwa ili:

(i) Kuchochea udadisi au fikra kuhusu suala linaloangaziwa.

(ii) Kusisitiza jambo linalozungumziwa.

## <u>MAANA YA KITAMATHALI NA MAANA YA KIJUUJUU KATIKA USHAIRI</u>

Baadhi ya mashairi huwa na maana ya kijuujuu na maana ya kitamathali. Maana ya kijuujuu ya shairi ni maana ya nje ya shairi. Maana ya kitamathali ni maana ya ndani ya shairi.

**Tazama shairi hili.**

Siafu ni hatari, wanapoteseka, huungana
Mikono hushikana, huapa, kupinga madhila
Ari huwajaa, nafsini, na roho zao dhaifu
Wana ghadhabu, masaibu, yawakaba koo.

### Maana ya kijuujuu ya shairi hili ni kuhusu siafu

Mshairi anasema kuwa siafu ni hatari wanapoteseka na wao huungana na kushikana mikono. Siafu hawa wana ghadhabu kutokana na masaibu yanayowaandama.

### Maana ya kitamathali (maana ya ndani)

Shairi hili linaeleza kuhusu binadamu. Mtunzi wa shairi anaeleza kuwa binadamu hawa wanapoteseka, wao huungana na kushirikiana ili kuyakataa maovu wanayofanyiwa. Binadamu hawa wana hasira kuto-kana na matatizo yanayowakabili.

Maana ya kijuujuu katika shairi hueleweka kwa urahisi kwa kuwa huhusisha mambo tunayoyafahamu. Maana ya kitamathali si wazi na maarifa huhitajika ili kuweza kuifahamu.

# SARUFI

## SAUTI

## KONSONANTI

Hizi ni sauti ambazo hutamkwa wakati hewa inayotoka kwenye mapafu inapozuiliwa na ala mbalimbali za kutamka sauti.

Utamkaji wa konsonanti hutegemea vigezo vifuatavyo.

(a) Mahali hewa inapozuiliwa

(b) Jinsi hewa inavyozuiliwa

(c) Mtetemeko katika nyuzi za sauti

Jedwali lifuatalo linaonyesha utamkaji wa sauti kwa kuzingatia vigezo hivyo vitatu vilivyotajwa.

| JINSI HEWA INAVYOZUILIWA | MAHALI HEWA INAPOZUILIWA | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Mdomo | Meno | Ufizi | Mdomo na meno | Kaakaa gumu | Kaakaa laini | Koo |
| Vipasuo sighuna ghuna | p b | | t d | | | k g | |
| Vikwamizosighuna ghuna | | th dh | s z | f v | sh | gh | h |
| Vipasuo kwamizo sighuna ghuna | | | | | ch j | | |
| Nazali sighuna ghuna | m | | n | | ny | ng' | |
| Kitambaza sighuna ghuna | | | l | | | | |
| Kimadende sighuna ghuna | | | r | | | | |
| Viyeyusho sighuna ghuna | w | | | | y | | |

Kutokana na jedwali hili, mwanafunzi atakuwa na uwezo wa kueleza sifa za sauti yoyote bila taabu.

**Mifano ya maswali**

(a) **Eleza sifa za sauti /d/**

(i) Hii ni sauti ya ufizi.

(ii) Sauti hii inapotamkwa mtetemeko wa sauti hushuhudiwa.

(iii) Hii ni sauti aina ya kipasuo.

(b) **Swali la KCSE 2018**

Andika sauti zenye sifa zifuatazo:

(i) kipasuo ghuna cha mdomoni.

Jibu ni /b/

(ii) kikwamizo sighuna cha kaakaa gumu

Jibu ni /sh/

(iii) nazali ya ufizi

Jibu ni /n/

## IRABU

Hii ni sauti ambayo hutamkwa bila ya hewa kuzuiliwa na ala mbali-mbali za kutamkia sauti.

Tofauti iliyopo kati ya utamkaji wa irabu na utamkaji wa konsonanti ni kuwa katika utamkaji wa konsonanti, hewa huzuiliwa na ala mbali-mbali za utamkaji wa sauti zilizo kinywani au puani. Katika utamkaji wa irabu hewa kutoka mapafuni hutokea kinywani bila kuzuiliwa na ala mbalimbali za utamkaji.


Utamkaji wa irabu hutegemea vigezo vifuatavyo:

(a) Sehemu ya ulimi. Ulimi huwa mbele au nyuma.

(b) Mkao wa midomo. Huwa imetandazwa au kuviringwa.

(c) Mwinuko wa ulimi. Ulimi huwa chini, kati au juu.

Mchoro unaofuata unaonyesha utamkaji wa irabu kwa kuzingatia vigezo vilivyojadiliwa hapo juu.




Irabu **o** na **u** zinapotamkwa midomo huwa mviringo. Vilevile ulimi huwa nyuma. Irabu **a**, **e** na **i** zinapotamkwa midomo huwa imeta-ndazwa. Vilevile ulimi husogezwa na kuwa mbele kinywani.

Irabu **e** na **o** ni za kati hali irabu **i** na **u** ni za juu. (zinapotamkwa, ulimi huinuliwa na kuwa juu kinywani)

**Swali la KCSE 2012**

(a)Andika vitamkwa vyenye sifa zifuatazo:

(i) irabu ya mbele, wastani

Jibu ni e

(ii) kipasuo ghuna cha kaakaa laini

Jibu ni /g/

## VIPASHIO VYA LUGHA

Hivi ni vinne. Navyo ni:

### Sauti

Ni kipashio cha chini kabisa katika lugha. Mfano /p/

### Silabi

Ni fungu moja la sauti linalotokana na muungano wa konsonanti na irabu. Mfano, pa.

### Neno


Silabi zinapounganishwa pamoja huunda maneno.

Mfano wa maneno ni papa, baba na mama.

## Sentensi

Hiki ni kipashio cha juu kabisa cha lugha. Hutokana na kuunganisha maneno mbalimbali.

Baba anasoma gazeti.




**Swali**

Taja vipashio viwili vya juu vya lugha.

**Jibu ni:**

neno kwa mfano papa

sentensi kwa mfano, Watoto wanacheza.

## Ala sogezi na ala tuli

**Ala sogezi** ni ala za kutamka sauti ambazo husogeasogea wakati

wa kutamka sauti. Mifano ya ala sogezi ni ulimi na midomo. **Ala tuli** ni ala ambazo hazisogei wakati wa kutamka sauti. Mifano ya ala tuli ni meno, ufizi, kaakaa gumu na kaakaa laini.

## Silabi wazi na silabi funge

**Silabi wazi** ni silabi inayoishia kwa irabu. Mfano pa katika neno papa. **Silabi funge** ni ile inayoishia kwa konsonanti. Mfano, lum katika neno maalum.

## Kiimbo

Ni kupanda na kushuka kwa sauti kunakotokea binadamu anapoongea. Kiimbo hutumiwa kutekeleza majukumu mbalimbali.

**Majukumu hayo ni:**

(a) Kuonyesha sentensi agizi au za amri.

Funga majani matano matano kwa kila aina.

(b) Hudhihirisha sentensi za maswali.

Utakuja kwetu lini?

(c) Hutumiwa kubainisha sentensi za ombi.

Niazime kalamu yako.

(d) Huonyesha sentensi zinazodhihirisha mshangao.

Lo! Vitimbi vyake vinakera.

(e) Hutumika kuonyesha kauli za taarifa.

Mama atakuja kesho asubuhi.

## SHADDA

Ni mkazo katika neno. Katika utamkaji wa maneno kuna silabi ambayo hutiliwa mkazo. Kwa kawaida shadda huwekwa kwenye silabi ya pili kutoka mwisho katika neno.

**Swali**

(a) Bainisha silabi zinazowekwa shadda katika maneno yafuatayo.

(i) wanaume

wana'ume silabi **u**

(ii) mkutano

mku'tano silabi **ta**

## Sauti mwambatano na silabi mwambatano

Sauti mwambatano ni sauti ambayo ina konsonanti mbili na zaidi ambazo zinafuatana bila ya irabu.

**Mfano**

**nyw** katika neno kunywa

Silabi mwambatano ni silabi iliyo na konsonanti mbili au zaidi zikifuatana pamoja na irabu.

**Mfano, swa** katika neno swali.

**Swali la KCSE 2013**

(a) (i) Eleza maana ya sauti mwambatano.

(ii) Andika sauti mwambatano inayotamkiwa kwenye ufizi.

Sauti mwambatano za ufizi ni nd(ndizi), st(stadi) na sl,(sleti).

## Silabi

Silabi ni fungu moja la sauti linalotokana na muungano wa konsonanti na irabu.

## Miundo ya silabi

Kuna miundo mbalimbali ya silabi. Miundo hiyo ni pamoja na:

(a) Konsonanti na irabu

**Mfano,** pa, da, ta na za.

(b) Konsonanti, konsonanti na irabu

Mfano, **pwa** (pwagu) na **gwa** (pigwa)

(c) Konsonanti, konsonanti, konsonanti na irabu.

**Mfano,** nywa (kunywa)

(d) Irabu pekee

Irabu zote za kiswahili ni silabi.

a, e, i, o, u

(e) Konsonanti, irabu na konsonanti.

Mfano, lum (maalum)

(f) Konsonanti pekee

Mfano m (neno mbu)

**SWALI LA KCSE 2014**

(a) (i) Eleza maana ya silabi.

(ii) Andika neno lenye muundo ufuatao.

Irabu +Konsonanti + Konsonanti + Irabu

ibra

**SWALI LA KCSE 2017**

1. Andika maneno yenye miundo ifuatayo.

(i) Konsonanti, konsonanti, konsonanti, irabu, konsonanti, irabu.

Jibu ni mtwana

(ii) Konsonanti, konsonanti, irabu, konsonanti, irabu

nguzo

Aina za sauti kwa kuzingatia namna hewa inavyozuiliwa.

(i) **Vipasuo**

Hizi ni sauti ambazo hutamkwa baada ya hewa kuzuiliwa na ala za utamkaji na kisha inaachiliwa ghafla.

Mifano ya vipasuo ni /p/, /b/, /t/, /d/, /k/ na /g/.

(ii) **Vikwamizo/ Vikwaruzo**

Hizi ni sauti ambazo hutamkwa wakati ala za kutamkia sauti zinapokaribiana sana bila kugusana. Hewa hulazimishwa kupita na hivyo inatoka kwa njia ya kukwama.

Mifano ya sauti hizi ni /s/, /z/, /f/, /v/, /sh/, /th/, /dh/, /gh/ na /h/.

(iii) **Vipasuo kwamizo**

Hizi ni sauti ambazo zinapotamkwa kunatokea mkwaruzo na mpasuko hafifu.

Sauti hizi ni /ch/ na /j/.

(iv) **Nazali/ving'ong'o**

Zinapotamkwa, ala za kutamka huzuia hewa isipite kinywani na hivyo hewa ile hutokea puani. Sauti hizi ni /m/, /n/, /ny/ na /ng'/.

(v) **Kimadende**

Hii ni konsonanti ambayo hutamkwa kwa ncha ya ulimi kupiga-piga ufizi kabla ya hewa kuachiliwa kutoka kinywani. Konsonanti hii ni /r/.

(vi) **Kitambaza**

Hutamkwa wakati ncha ya ulimi inapokutanishwa na ufizi na kisha hewa inaachiliwa mara moja. Sauti hii ni /l/.

(vii) **Viyeyusho/Nusu irabu**

Hizi ni sauti ambazo hutamkwa kwa ala za kutamkia kukaribiana bila kugusana. Kwa hiyo, hewa hutoka bila kuzuiliwa.

Sauti hizi ni /w/ na /y/.

## VIJALIZO

Kijalizo ni neno ambalo huja baada ya kitenzi kishirikishi.

**Mfano**

Mtoto yule ni mdogo.

Mdogo ni kijalizo kwa sababu linakuja baada ya kitenzi kishirikishi ambacho ni **ni**.

Yeye angali uwanjani.

Neno uwanjani ni kijalizo kwa kuwa linakuja baada ya kitenzi kishirikishi ambacho ni **angali**.

## VITATE NA VISAWE

Vitate ni maneno ambayo yana sauti zinazokaribiana na hivyo hukanganya wakati wa utamkaji.

**Mifano ya maneno haya ni:**

vuja rithi ajali

fuja ridhi ajari

Mwanafunzi anapoambiwa atunge sentensi moja akitumia vitate, ahakikishe kwamba maana tofauti ya maneno hayo inadhihirika katika sentensi.

**Swali la KCSE 2015**

Tunga sentensi moja ili kutofautisha maana ya vito na fito. Katika swali hili, maana ya maneno haya idhihirike waziwazi.

Vito vya thamani vya mfalme vilihifadhiwa katika nyumba iliyotengezwa kwa fito.

**VISAWE (SINONIMU)**

Haya ni maneno tofauti ambayo huwa na maana sawa.

Mfano, kisawe cha kiambaza ni ukuta.

kazi – ajira kompyuta - tarakilishi

mdanganyifu – mwongo pakacha – kitasi

mchukuzi – hamali kero – adha

mdomo - kinywa

**Swali**

Andika visawe vya kauli zilizopigiwa mstari.

**Daktari** alimpa **mgonjwa dawa**.

Jawabu sahihi ni

**Tabibu** alimpa **muwele maponyo**.

**Swali la KCSE 2016**

Andika visawe vya maneno yaliyopigiwa mstari.

**Kiambaza** kilimuumiza **ghulamu** alipokuwa **akipanda.**

Jawabu sahihi ni,

**Ukuta** ulimuumiza **mvulana** alipokuwa **akikwea**.

## NYAKATI NA HALI

Kuna viambishi mbalimbali ambavyo hutumiwa kuonyesha nyakati na hali mbalimbali.

### Nyakati

#### Wakati uliopo

Wakati uliopo huonyeshwa na kiambishi **na.**

**Mfano,** Mtoto a**na**cheza uwanjani.

Wanafunzi wa**na**soma.

#### Wakati ujao

Kiambishi kinachotumiwa kuonyesha wakati ujao ni **ta**.

Walimu wa**ta**sahihisha madaftari.

Asha a**ta**soma kitabu.

**Wakati uliopita**

Kiambishi **li** huonyesha wakati uliopita.

Zawadi zi**li**tolewa na wageni.

Ni**li**safirisha mizigo hiyo.

**Wakati usiodhihirika**

Kiambishi '**a**' hutumiwa kubainisha wakati usiodhihirika.

**Mfano**

Atieno **a**lima shambani.

**Hali**

**Hali ya mazoea**

Huonyeshwa na kiambishi **hu**.

Wapishi **hu**pika chakula kitamu.

Wazazi **hu**watunza watoto wao.

**Hali timilifu**

Kiambishi **me** hutumika kuonyesha hali timilifu.

Mkutano u**me**kamilika vizuri.

Shule zi**me**funguliwa mapema.

Mifano ya maswali katika mtihani wa kitaifa.

**KCSE 2021**

Andika sentensi ifuatayo katika wakati uliopita hali ya mazoea.

Bibi atawashauri vijana kuhusu umuhimu wa michezo.

Jawabu

Bibi alikuwa akiwashauri vijana kuhusu umuhimu wa michezo.

**KCSE 2018**

Andika sentensi ifuatayo katika wakati ujao hali ya mazoea.

Barabara nyingi zimesakafiwa.

Jawabu

Barabara nyingi zitakuwa zikisakafiwa.

## <u>NGELI</u>

Ni mfumo wa kuweka nomino katika vikundi mbalimbali kwa kuzingatia viwakilishi vya nomino hizo. Lugha ya Kiswahili ina ngeli mbalimbali.

(a) **Ngeli ya A – WA**

Hii ni ngeli ya nomino za vitu vyote vilivyo na uhai. Hizi hujumuisha watu, wadudu, wanyama, ndege na vitu vingine vyote vilivyo na uhai. Nomino hizi huanza kwa kiambishi **a** katika umoja na **wa** katika wingi. Baadhi ya maneno katika ngeli hii ni kama mkulima, mbuzi, kuku, kipepeo, seneta, mtoto, malaika, kaa na siafu.

**Mifano katika sentensi:**

Mbuzi **a**mekata kamba.

Mbuzi **wa**mekata kamba.

Mwalimu **a**nafundisha darasani.

Walimu **wa**nafundisha madarasani.

Miundo ya nomino katika ngeli ya A – WA

(a) ki – vi mfano kipepeo – vipepeo

m - wa mfano mdudu - wadudu

Ɵ – ma mfano nyani – manyani

Ɵ – Ɵ mfano malaika – malaika

**Swali la KCSE 2017**

Onyesha miundo miwili ya nomino katika ngeli ya A – WA.

**Ngeli ya LI – YA**

Hushirikisha nomino nyingi ambazo hazina uhai. Huchukua kiambishi

**li** katika umoja na **ya** katika wingi. Mifano ya baadhi ya nomino katika

ngeli ya LI – YA ni:

jani, jicho, sikio, jawabu, jengo, sanduku, jiwe na chungwa

**Mifano katika sentensi**

Jani **li**lianguka majini.

Majani **ya**lianguka majini.

Jengo **li**lilojengwa limebomoka.

Majengo **ya**liyojengwa yamebomoka.

Miundo ya nomino katika ngeli ya LI – YA.

ji – ma mfano jiwe – mawe

Ѳ – ma mfano sikio – masikio

**Ngeli ya KI – VI**

Nomino katika ngeli hii huchukua kiambishi **ki** katika umoja na **vi** katika wingi.

Baadhi ya nomino hizi ni kijiko, chalo, chandarua, chambo, kijiji, chuo na kisima.

**Mifano katika sentensi**

Kijiko **ki**litumiwa na mpishi.

Vijiko **vi**litumiwa na wapishi.

Cheti hicho **ki**limwezesha kupata kazi.

Vyeti hivyo **vi**liwawezesha kupata kazi.

Miundo ya nomino katika ngeli ya KI – VI

ki – vi mfano kijiko vijiko

ch – vy mfano cheti vyeti

**Ngeli ya U – I**

Nomino katika ngeli hii huchukua kiambishi **u** katika umoja na **i** katika wingi ili kuleta upatanisho wa kisarufi.

Baadhi ya nomino katika ngeli hii ni:

mti, mkono, mmea, mleo, mlio na mlima.

**Mifano katika sentensi**

Mti **u**likatwa jana.

Miti ilikatwa jana.

Mlima **u**na theluji.

Milima **i**na theluji.

Miundo ya nomino katika ngeli ya U – I

m – mi mfano mlima milima

mu – mi mfano muktadha miktadha

mw – mi mfano mwereka miereka

**Ngeli ya YA – YA**

Nomino katika ngeli hii hurejelea vitu visivyohesabika. Asilimia kubwa ya nomino hizi huanza na kiambishi ma. Kiambishi cha upatanisho ni **ya** katika umoja na wingi.

Baadhi ya nomino katika ngeli hii ni mate, maji, maadili, maakuli na madaraka.

Mifano katika sentensi.

Maji **ya**limwagika.

Maji **ya**limwagika.

Maziwa **ya**mechemka.

Maziwa **ya**mechemka.

Miundo ya nomino katika ngeli ya YA – YA

Ө – Ө Mfano mate mate

**Ngeli ya I – ZI**

Nomino katika ngeli ya I – ZI huchukua kiambishi **i** katika umoja na **zi** katika wingi. Nomino hizi hazibadiliki katika umoja na wingi.

Baadhi ya nomino katika ngeli hii ni nyumba, nguzo, njia, nyundo, nyungu, simu, notisi, maikrowevu, helmeti, hesabu na taarifa.

Maneno mengi yaliyokopwa kutoka lugha nyinginezo hupatikana katika ngeli hii.

**Mifano katika sentensi**

Nyumba **i**libomoka.

Nyumba **zi**libomoka.

Notisi **i**metolewa.

Notisi **zi**metolewa.

Miundo ya nomino katika ngeli ya I – ZI

| | Umoja | wingi |
|---|---|---|
| Ө – Ө mfano | notisi | notisi |

**Ngeli ya U – ZI**

Nomino katika ngeli ya U – ZI huchukua kiambishi **u** katika umoja na **zi** katika wingi ili kuleta upatanisho wa kisarufi.

Baadhi ya nomino katika ngeli hii ni, ukuta, ufagio, unyeleo, wimbo, wembe, uzi, upongoo, unywele, unyasi, waya, wayo na ukucha.

**Mifano katika sentensi**

Waya **u**mekatika.

Nyaya **zi**mekatika.

Ukuta **u**mebomoka.

Kuta **zi**mebomoka.

Miundo ya nomino katika ngeli ya U – ZI

| | | |
|---|---|---|
| u – Ө mfano | ukuta | kuta |
| Ө – ny | uzi | nyuzi |

**Ngeli ya U – YA**

Kiambishi **u** hutumika katika umoja na **ya** katika wingi ili kuleta upatanisho wa kisarufi. Baadhi ya nomino katika ngeli hii ni ugonjwa, ulezi, uwele na unyoya.

**Mifano katika sentensi**

Ugonjwa **u**liwaathiri wengi.

Magonjwa **ya**liwaathiri wengi.

Unyoya **u**litumiwa na mtoto

Manyoya **ya**litumiwa na watoto.

Miundo ya nomino katika ngeli ya U – YA

u – ma mfano unyoya manyoya

**Ngeli ya U – U**

Kiambishi cha upatanisho katika ngeli hii ni **u** katika umoja na wingi. Nomino hizi hazibadiliki katika umoja na wingi.

Baadhi ya nomino katika ngeli hii ni unyevu, unyonge, upanzi, utandawazi, wahka, wajihi na wakfu.

**Mifano katika sentensi**

Utandawazi **u**meimarisha mawasiliano.

Utandawazi **u**meimarisha mawasiliano.

Miundo ya nomino katika ngeli ya U – U

Ɵ – Ɵ mfano unyevu unyevu

**Ngeli ya I – I**

Nomino katika ngeli hii huchukua kiambishi **i** katika umoja na wingi.

Baadhi ya nomino katika ngeli hii ni chai, choa, chokoleti, imani, intaneti, inijili, kande na miwani.

**Mifano katika sentensi**

Chai **i**menywewa.

Chai **i**menywewa.

Miwani **i**menunuliwa.

Miwani **i**menunuliwa.

**Ngeli ya KU**

Kiambishi kipatanishi cha ngeli hii ni **ku**.

Nomino katika ngeli hii hutanguliziwa na kiambishi ku. Kiambishi **ku** huongezwa kwenye mizizi ya vitenzi.

**Mifano katika sentensi**

Kutembea kwake **ku**napendeza.

Kutembea kwa muda mrefu **ku**nachosha.

**Ngeli ya PA KU MU**

Hii ni ngeli ya mahali.

PA – Huonyesha mahali maalum na panapodhihirika.

**Mfano** Mahali hapa **pa**navutia.

Mahali hapa **pa**na siafu.

KU – Hutumiwa kuonyesha mahali kusikodhihirika.

Mahali huku **ku**navutia.

Mahali huku **ku**na siafu.

MU – Huonyesha mahali ndani.

Mahali humu **m**navutia.

Mahali humu **m**na siafu.

Viambishi hivi vya ngeli havifai kuchanganywa.

Sentensi zifuatazo si sahihi.

1. *Mahali huku mnavutia.
2. *Mahali hapa kunavutia.

Sentensi sahihi ni:

1 (a)Mahali huku kunavutia.

au

(b) Mahali humu mnavutia.

2 (a) Mahali hapa panavutia.

au

(b) Mahali huku kunavutia.

**Swali la KCSE 2018**

Nomino zifuatazo zimo katika ngeli gani?

(i) ugwe U – ZI

(ii) limau LI – YA

**SWALI LA KCSE 2014**

Nomino zifuatazo zimo katika ngeli gani?

(i) Furaha I – I

(ii) Nyasi U – ZI

**UMOJA NA WINGI**

Umoja na wingi katika sentensi hutegemea kwa kiasi kikubwa ngeli husika.

Inapendekezwa kwamba mwanafunzi achunguze sentensi ipo katika ngeli gani kabla ya kuigeuza iwe katika wingi. Vilevile achunguze kama nomino zitabadilika na kuwa katika hali ya wingi.

**Mifano**

**Swali la KCSE 2017**

Igeuze sentensi ifuatayo iwe katika hali ya umoja.

Maseremala walilainisha mbao hizo wakatutengenezea meza.

**Jawabu**

Seremala alilainisha ubao huo akanitengenezea meza.

**Swali la KCSE 2007**

Andika kwa wingi:

Nyundo hii imevunjika mpini wake.

**Jawabu**

Nyundo hizi zimevunjika mipini yake.

**Swali**

Andika sentensi ifuatayo katika umoja.

Nyua walizojenga hapa zimesaidia kukabiliana na wahalifu hao.

**Jawabu**

Ua aliojenga hapa umesaidia kukabiliana na mhalifu huyo.

**Swali ya KCSE 2014**

Andika sentensi ifuatayo katika umoja.

Hao wenyewe hawakuzingatia mafunzo ya lishe bora.

**Jawabu**

Huyo mwenyewe hakuzingatia funzo la lishe bora.

**Mifano zaidi.**

Unataka cheti cha kukusaidia? (umoja)

Mnataka vyeti vya kuwasaidia? (wingi)

Ukwato wa mnyama hunifaidi. (umoja)

Kwato za wanyama hutufaidi. (wingi)

Koshi lake lilivaliwa na fundi. (umoja)

Makoshi yao yalivaliwa na mafundi (wingi)

Ngoma ilipigwa na mchezaji akafurahi. (umoja)

Ngoma zilipigwa na wachezaji wakafurahi. (wingi)

Nyani alichupa kutoka mti ule. (umoja)

Manyani walichupa kutoka miti ile. (wingi)

## HALI YA KUKANUSHA

Kukanusha ni ile hali ya kupinga hali fulani. Katika kukanusha sentensi ni muhimu kuangalia viambishi vya nyakati na hali vilivyotumiwa.

**Mifano**

Mimi nitacheza.

**kukanusha**

Mimi sitacheza.

Juma alipigwa.

**kukanusha**

Juma hakupigwa.

**Swali la KCSE 2018**

Kanusha sentensi ifuatayo.

Mkulima anahitaji magunia haya.

**Jawabu**

Mkulima hahitaji magunia haya.

**Swali la KCSE 2014**

Wanafunzi waliingia darasani, wakatoa vitabu wakaanza kusoma.

Wanafunzi hawakuingia darasani, hawakutoa vitabu wala hawakuanza kusoma.

Kuna viambishi mbalimbali vinavyotumiwa katika kukanusha nyakati na hali mbalimbali.

### Wakati uliopo

Kiambishi **si** na **ha** hutumika kukanusha wakati uliopo.

**Mfano**

Sisi tunasoma.

Sisi hatusomi.

Mimi ninakimbia.

Mimi sikimbii.

### Wakati ujao

Viambishi vya kukanusha wakati ujao ni **ha** na **si**.

Yeye atapanda miche.

Yeye hatapanda miche.

Mimi nitapika chakula.

Mimi sitapika chakula.

Wazazi watawatembelea.

Wazazi hawatawatembelea.

**Wakati uliopita**

Viambishi **si**, **ha** na **hu** hutumika kukanusha wakati uliopita.

Sisi tulisoma. Mimi nilikimbia.

Sisi hatukusoma. Mimi sikukimbia.

**Wakati usiodhihirika**

Kiambishi **ha** hutumika kukanusha wakati usiodhihirika.

Asha alima.

Asha halimi.

**Swali la KCSE 2011**

Kanusha sentensi ifuatayo.

Mgonjwa huyo alipona na kurejea nyumbani.

**jibu**

Mgonjwa huyo hakupona wala hakurejea nyumbani.

Viambishi **si**, **ha** na **hu** aghalabu hutumika katika ukanushaji.

**Mifano zaidi**

Ningalikuwa na pesa ningalinunua gari.

Nisingalikuwa na pesa nisingalinunua gari.

**Swali la KCSE 2008**

Kanusha:

Sisi tumemaliza kujenga nyumba ambayo ingalikuwa yake angalifurahi.

Sisi hatujamaliza kujenga nyumba ambayo isingalikuwa yake asingalifurahi.

## HALI YA KUYAKINISHA

Kuyakinisha ni kuandika sentensi katika hali isiyo ya kukanusha. Unapoyakinisha sentensi, unazigeuza ziwe katika hali isiyo ya kukanusha.

**Mifano**

Sisi hatusomi. Katika kuyakinisha sentensi yenyewe itakuwa, **Sisi tunasoma**.

**Mifano zaidi**

Wazazi hawakuwatembelea. (sentensi hii ipo katika hali ya kukanusha)

Wazazi waliwatembelea. (hali yakinishi)

**Swali la KCSE 2016**

Askari wasipopiga doria wala kushirikiana na raia hawatakuwa wametuhakikishia usalama. (yakinisha sentensi hii)

**Jawabu**

Askari wakipiga doria na kushirikiana na raia watakuwa wametuhakikishia usalama.

**Swali la KCSE 2010**

Andika sentensi ifuatayo katika hali yakinishi.

Usingeacha masomo, usingetaabika vile.

Ungeacha masomo, ungetaabika vile.

**Mifano zaidi**

Mgonjwa huyo hakupona wala hakurejea nyumbani.

Mgonjwa huyo alipona na kurejea nyumbani. (hali yakinishi)

Mkulima hahitaji magunia haya.

Mkulima anahitaji magunia haya. (hali yakinishi)

## UAKIFISHAJI

Hii ni mada ya sarufi ambayo hudhamiria kuchunguza ikiwa mwanafunzi:

(a) ana uwezo wa kutambua viakifishi mbalimbali.

(b) atatumia viakifishi vyenyewe kwa njia sahihi.

(c) ataweza kuakifisha sentensi kwa njia sahihi.

Mtindo wa kutahini mada ya uakifishaji ni kama ufuatao.

1 Eleza huku ukitoa mfano matumizi mawili ya kistari kifupi.

2 Akifisha:

Nitakuja kesho asubuhi Thairu alisema.

**Viakifishi mbalimbali**

(a) **Alama za mtajo/ Usemi/ Kunukuu (“ “)**

**Matumizi yake**

(i) Hutumiwa kufungia maneno halisi ya msemaji.

**Mfano**

Kamau alisema, “Nitakuja kesho.”

(ii) Hutumiwa kuonyesha majina ya vipindi vya redio au anwani inapotokea katika sentensi. Mfano,

Alitazama kipindi cha “Maria” jana jioni.

(iii) Huonyesha maneno ya lugha nyingine.

Waliagiza “githeri” walipoingia hotelini.

(iv) Hutumiwa kuonyesha maneno yaliyotumika kwa kinaya.

Juma “alipita” mtihani kwelikweli kwani alipata alama kumi kwa mia saba.

(b) **Ritifaa/ Kibainishi (’)**

(i) Hutumiwa kuonyesha kwamba kuna silabi ambazo zimeachwa katika neno.

‘tachukua atachukua

(ii) Hutumika katika maneno yenye ving’ong’o.

**Mfano,** ng’ombe, ng’ara na ng’ambo.

(c) **Nukta/ Kitone/ Kikomo (.)**

(i) Huwekwa mwishoni mwa sentensi.

Kiptoo amepita mtihani.

(ii) Hutumiwa katika kutenga pesa.

Alinunua shati hilo shilingi 650. 50.

(iii) Unapofupisha maneno, kitone hutumiwa.

K .M. (kwa mfano)

S.L.P. (Sanduku la posta)

(d) **Nukta mbili/ Nukta pacha/Koloni (:)**

(i) Hutumiwa katika kuorodhesha vitu.

**Mfano**

Alinunua bidhaa hizi alipoenda sokoni: sukari, chumvi na maziwa.

(ii) Katika mahojiano au mazungumzo nukta mbili hutumiwa.

Moreno : U hali gani ndugu?

Asipo : Sina neno ndugu.

(iii) Hutenga saa na dakika.

Saa 8 :13

(e) **Nukta mkato (;)**

(i) Hutumika katika sentensi ili kutenganisha mawazo katika sentensi ndefu.

Wazee wa kijiji hicho walijitahidi sana; walielewa kwamba walikuwa nguzo katika ufanisi wa kijiji chenyewe.

(ii) Hutumiwa kumpumzisha msomaji katika sentensi iliyo ndefu.

Ugonjwa wa Covid-19 uliwaathiri Wakenya pakubwa; biashara pamoja na taasisi za mafundisho zilifungwa ili kuzuia kusambaa kwa ugonjwa wenyewe.

(f) **Koma (,)**

(i) Hutumika katika anwani.

S.L.P. 164,

RUMURUTI.

(ii) Hutumiwa ili kumpumzisha msomaji katika sentensi.

Nililala mapema jana, nilikuwa nimechoka tiki.

(iii) Katika orodha, alama ya koma hutumiwa.

Alinunua sukari, chumvi, maziwa na mayai.

(g) **Mabano/ parandesi. ( ( ) )**

(i) Hutumiwa katika kufungia nambari au herufi.

**Mifano,** (i) na (a)

(ii) Huonyesha taarifa za nyongeza katika sentensi.

Wazazi wake Aisha (wakulima) walipata hasara kubwa (msimu uliopita) kutokana na kiangazi.

(h) **Kistari kifupi ( - )**

(i) Unapotenganisha silabi, kistari kifupi hutumiwa.

ma- la- i- ka

(ii) Kuonyesha kipindi cha wakati.

2019 – 2021

(iii) Hutumiwa katika maneno yaliyounganishwa.

Chapa-asili

(iv) Mwishoni mwa pambizo ikiwa neno halijakamilika alama hii hutumika.

Wazee wote katika mtaa huu wali-

washukuru wakazi hao.

(v) Hudokeza pahali pa viambishi vya ngeli katika maneno.

- baya, - ote, -enu.

(i) **Kistari kirefu** ——

(i) **Huonyesha** taarifa za nyongeza katika sentensi.

Jatu na Milo walijiunga na chuo cha—Ufanisi kilikuwa ni chuo kilichoasisiwa na kiongozi wa kwanza nchini Tupo.

(j) **Mkwaju/Mshazari (/)**

(i) Hutumika katika hali ambapo vitu viwili vinaweza kuhusika.

Mbunge/ Waziri ataruhusiwa kuingia.

(ii) Hutumika katika uandishi wa tarehe.

22/04/2021

(iii) Hutumika katika kumbukumbu za mikutano.

KUMB. 4/4/2021

(k) **Mstari__________**

(i) Huwekwa chini ya anwani.

**Mfano**

**<u>UMUHIMU WA KUPANDA MITI</u>**

(ii) Hutumika katika sentensi unapotaka kusisitiza.

<u>Utawala mbaya</u> umeiponza nchi yetu.

(l) **Kinyota (*)**

(i) Hutumika katika kuonyesha kuwa kuna taarifa za ziada ambazo zimeolewa katika neno lililowekwa alama hii.

Ugonjwa wa *Covid-19 uliathiri ulimwengu mzima. (*Covid–19 ni ugonjwa ambao kitovu chake ni taifa la Uchina, jiji la Wuhan)

(ii) Huonyesha kwamba sentensi ina makosa ya kisarufi.

*Mzee hiki kimepata zawadi.

(iii) Ikiwa neno limeendelezwa visivyo, alama hii hutumika.

*shakula.

**Swali la KCSE 2009**

Huku ukitoa mifano mwafaka onyesha matumizi mawili ya kinyota (*) katika sarufi ya Kiswahili.

(m) **Alama hisi (!)**

Hutumiwa kuthibitisha hisia kama mshangao, huzuni, majonzi, furaha na masikitiko.

**Mifano** Lo! Musa ni mwizi. (mshangao)

Hoyee! Timu yetu imeshinda. (furaha)

(n) **Alama ya kiulizi (?)**

Huonyesha kwamba kuna swali.

Watoto waliwasili wangapi?

(o) **Matumizi ya herufi kubwa**

(i) Hutangulizwa mwanzoni mwa sentensi.

Wanafunzi walipita mtihani.

(ii) Katika majina ya miji.

Nairobi ni jiji kuu la Kenya.

(iii) Unapoandika majina ya vitabu vitakatifu.

Wakristo walisoma Bibilia walipokuwa kanisani.

(iv) Mwanzoni mwa majina ya miezi.

Mei, Desemba na Machi.

Alipokea barua hiyo mwezi wa Mei.

(v) Unapoandika majina ya watu.

Kiptoo, Munene, Mary na Elizabeth.

(vi) Mwanzoni mwa majina ya nchi.

Kenya, Uganda na Tanzania ni nchi zinazotumia lugha ya Kiswahili.

(vii) Unapoandika majina ya lugha mbalimbali.

Kiswahili, Kiingereza, Kijerumani na Kifaransa.

(viii) Unapoandika siku za juma. Alhamisi, Jumatatu na Ijumaa.

Wageni waliondoka Alhamisi.

**ZOEZI**

Eleza matumizi ya alama zifuatazo.

(a)Herufi za mlazo.

(b)Alama za mdokezo.

**Swali la KCSE 2011**

SWALI 1. Akifisha kifungu kifuatacho:

Mzee alimwambia mwanawe njoo nikupeleke kwa babu yako angalau umjue mtoto aliuliza nani babu?

Mzee alimwambia mwanawe, “Njoo nikupeleke kwa babu yako angalau umjue.”

Mtoto aliuliza, “Nani babu?”

**Swali la KCSE 2017**

SWALI 2. Alama za mtajo hutumiwa kufungia maneno halisi ya msemaji. Tunga sentensi mbili kuonyesha matumizi mengine mawili ya alama za mtajo.

(i) “Tete na tete” ni istilahi muhimu katika muziki. (Kuonyesha maneno ya kigeni)

(ii) Tulitazama kipindi cha “Zora” jana usiku.

## UDOGO, WASTANI NA UKUBWA

Nomino za Kiswahili zinaweza zikawa katika hali tatu; udogo, wastani na ukubwa. Kwa kawaida nomino huwa katika hali ya wastani. Hata hivyo nomino hizi zinaweza zikawa katika hali ya udogo au ya ukubwa.

### Hali ya udogo

Hali ya udogo huonyeshwa na kiambishi **ki** au **kiji** katika umoja na **vi** au **viji** katika wingi. Sentensi yoyote inapogeuzwa na kuwa katika hali ya udogo, sentensi hiyo itachukua viambishi katika ngeli ya KI – VI. Mwanafunzi atilie maana upatanisho wa kisarufi wa sentensi yenyewe.

**Mifano**

| Wastani | Udogo |
|---|---|
| kitabu | kijitabu |
| mzee | kizee |
| mbuzi | kibuzi |
| mtoto | kitoto |
| kiatu | kijiatu |
| mpira | kipira |
| sahani | kisahani |
| nguo | kiguo |
| duka | kiduka |

(i) Katika kuzigeuza nomino katika udogo baadhi ya nomino huongezwa **ki** mwanzoni mwa nomino hizo.

**Mifano**

| Wastani | Udogo |
|---|---|
| sufuria | kisufuria |
| meza | kimeza |
| saa | kisaa |

(ii) Kuna nomino ambazo huongezewa kiji iwapo nomino zenyewe zipo katika ngeli ya KI – VI.

**Mifano**

| Wastani | Udogo |
|---|---|
| kitabu | kijitabu |
| kikombe | kijikombe |
| kisu | kijisu |

(ii) Baadhi ya herufi huondelewa mwanzoni na kisha kiambishi ki kuongezwa.

**Mifano**

| Wastani | Udogo | Wingi |
|---|---|---|
| mpira | kipira | vipira |
| mbuzi | kibuzi | vibuzi |
| nguo | kiguo | viguo |
| mkebe | kikebe | vikebe |

**Mifano katika sentensi**

Mbuzi huyu atachinjwa kesho. (wastani)

Kibuzi hiki kitachinjwa kesho. (udogo)

Ngoma hiyo yao iliibiwa na mwizi yule. (wastani)

Kigoma hicho chao kiliibiwa na kijizi kile. (udogo)

**Ukubwa wa nomino**

Aghalabu kiambishi **ji** hutumiwa kuonyesha ukubwa wa nomino. Kiambishi **ma** hutumika katika wingi.

**Mifano**

| Wastani | Ukubwa |
|---|---|
| sahani | jisahani |
| meza | jimeza |
| saa | jisaa |

Nomino zinapobadilishwa na kuwa katika hali ya ukubwa huwa

katika ngeli ya LI – YA.

Mabadiliko yanayotokea katika nomino.

(i) Baadhi ya nomino hupoteza silabi ili kuwa katika hali ya ukubwa.

| Wastani | Ukubwa |
|---|---|
| mbuzi | buzi |
| njia | jia |
| mpira | pira |
| ngoma | goma |

(ii) Kiambishi **ji** huongezwa katika nomino zilizo na kiambishi **ki**.

**Mifano**

| Wastani | Ukubwa |
|---|---|
| kikombe | jikombe |
| kichwa | Jichwa |

Katika mitihani, mwanafunzi atakabidhiwa sentensi ambazo atahitajika kuzigeuza katika hali ya udogo au ukubwa.

**Swali la KCSE 2018**

1.Andika sentensi ifuatayo katika hali ya ukubwa.

Nguo ambazo zinauzwa kwenye duka hilo zinavutia.

**ukubwa**

Maguo ambayo yanauzwa kwenye jiduka hilo yanavutia.

**Swali la KCSE 2017**

2. Andika sentensi ifuatayo katika hali ya ukubwa.

Ngoma hizo zao ziliibwa na  wezi wale.

**ukubwa**

Magoma hayo yao yaliibwa na majizi yale.

**Swali la KCSE 2013**

Andika sentensi ifuatayo katika hali ya udogo:

Madebe hayo yatasafirishwa pamoja na nyundo hizi.

**udogo**

Videbe hivyo vitasafirishwa pamoja na vijundo hivi.

## AINA ZA MANENO

## NOMINO

Nomino ni maneno ambayo hutambulisha jina la mtu, kitu, mahali na hali. Kuna aina mbalimbali za nomino katika lugha ya Kiswahili.

### Aina za nomino

**(i) Nomino dhahania**

Hizi ni nomino za vitu ambavyo hatuwezi kuvishika wala kuvigusa. Ni vitu ambavyo ni vya kuwaza.

Baadhi ya nomino dhahania ni wivu, ujinga, chuki na upendo.

**Mifano katika sentensi**

Alijawa na **chuki** kutokana na vitendo vyake.

**Upendo** wa mama hauna kipimo.

**(ii) Nomino za makundi**

Hizi huonyesha vitu vinavyopatikana katika mikusanyiko.

**Mifano,** umati wa watu, bunda la noti, bumba la nyuki na shada la maua.

**Mifano katika sentensi**

**Umati wa watu** ulihudhuria mkutano huo.

Waliweka **shada la maua** sakafuni.

**Mifano zaidi**

Chane la ndizi, tumbi la samaki, shuke la nafaka, robota la pamba, korija la vitambaa, kigaro cha wasegenyaji, kikosi cha askari, kilinge cha wachawi, kipeto cha barua, wingu la nzige, tita la kuni, kikonyo cha zabibu, kifungu cha matunda, pakacha la matunda, genge la wezi, kopo la maji, robota la pamba, kanzi la maharagwe, bunda la funguo, tonge la ugali, kifurushi cha pamba, shazi la nafaka, shungi la nywele, doti la leso, mtungo wa samaki, tumbi la samaki na thurea ya nyota.

**(iii) Nomino za vitenzi jina**

Hizi ni nomino ambazo hutokana na kuongeza kiambishi ku kwenye vitenzi.

**Mifano**

ku + cheza → kucheza (nomino ya kitenzi jina)

ku + lima → kulima (nomino ya kitenzi jina)

ku + cheka → kucheka (nomino ya kitenzi jina)

**Mifano katika sentensi**

Kucheza kwake kunavutia.

Kucheka kwake kunaudhi.

**(iv) Nomino za wingi**

Hurejelea nomino zinazopatikana katika wingi pekee.

**Mifano,** maji, damu, wino, mate na chai.

Maji hayakumwagika.

Chai ilikolea sukari.

**(v) Nomino za pekee**

Ni nomino ambazo huanza kwa herufi kubwa zinapotumika mahali popote katika sentensi.

Nomino hizi hushirikisha majina ya nchi, watu, vitabu vitakatifu, miji, miezi, siku za juma na majina ya lugha mbalimbali.

**Mifano**

Tanzania ni taifa lililo na watu wengi.

Kiswahili ni lugha inayosemwa na watu wengi nchini.

**(vi) Nomino za kawaida**

Hurejelea maneno ya kawaida ambayo huanza kwa herufi ndogo isipokuwa tu yanapotumiwa mwanzoni mwa sentensi.

**Mifano ni,** kiti, meza, ukuta, kitabu, dawati, kalamu, mzigo, simu na mtungi.

**Mifano katika sentensi**

**Mzigo** ule ni mzito.

Kobole amenunua **simu**.

Katika mitihani, maswali yatatokea katika mitindo miwili:

**Mtindo wa kwanza**

Kubainisha aina za nomino katika sentensi.

**Mfano**

Kiatu hiki ni cha Juma.

kiatu ni nomino ya kawaida

Juma ni nomino ya pekee

**Mtindo wa pili**

Kutunga sentensi kwa kutumia aina fulani za nomino.

**Mfano**

Tunga sentensi ukitumia nomino ya wingi na nomino ya makundi.

**Umati wa watu** ulibahatika kupata **maji**.

nomino ya makundi                nomino ya wingi

**Swali la KCSE 2018**

Mchuuzi alinunua mboga **zilizofungwa pamoja**. (tumia nomino ya jamii badala ya maneno yaliyopigiwa mstari)

Mchuuzi alinunua kifungu cha mboga.

**Swali la KCSE 2012**

Tunga sentensi moja yenye nomino dhahania na nomino ya jamii.

**Genge la wezi** lilijawa na **chuki** baada ya kusalitiwa na mwenzao.

nomino ya jamii          nomino dhahania

## VIHUSISHI

Haya ni maneno ambayo yanabainisha uhusiano baina ya vitu mbali-mbali.

Panya amejificha **mvunguni mwa** kitanda.

**Mvunguni mwa** ni kihusishi kinachodhihirisha uhusiano baina ya panya na kitanda.

**Aina za vihusishi**

**(a) Vihusishi vya mahali**

Hivi huonyesha uhusiano wa mahali.

**Mifano ya vihusishi hivi ni:** chini ya, juu ya, mvunguni mwa, mbele ya, nyuma ya na kando ya.

**Mifano katika sentensi**

Kitabu kimewekwa **juu ya** meza.

Walimu walisimama **mbele ya** jukwaa.

(b) **Vihusishi vya wakati**

Hutumiwa kuonyesha uhusiano wa wakati.

Baadhi ya vihusishi vya wakati ni halafu, baada ya, kisha, tangu na kabla ya.

**Mifano katika sentensi**

Mgomo ulianza **baada ya** mkutano kumalizika.

Alinawa mikono **kabla ya** kula.

**(c) Vihusishi vya kulinganisha**

Ni vihusishi ambavyo huleta dhana ya kulinganisha.

Baadhi ya vihusishi vya kulinganisha ni kuliko, zaidi ya na kama.

**Swali la KCSE 2016**

Ainisha vihusishi katika sentensi ifuatayo.

Baba alifika mapema kuliko wote halafu akaondoka.

kuliko ni kihusishi cha kulinganisha

halafu ni kihusishi cha wakati

**(d) Kihusishi na cha mtenda**

Ni kihusishi ambacho huonyesha mtendaji wa jambo pamoja na kitendo chenyewe.

Chakula kilipikwa **na** mpishi.

**na** ya mtenda

Samaki walibebwa **na** mvuvi.

**na** ya mtenda

**(e) Kihusishi cha 'a' unganifu**

Msingi wake umekitwa kwenye 'a' kutegemea ngeli husika. Hutambulisha uhusiano kati ya neno moja na lingine.

**Mifano**

Daftari **la** mwanafunzi limesahihishwa.

kihusishi cha 'a' unganifu

**Swali la KCSE 2015**

Tunga sentensi kuonyesha matumizi ya neno **kama** likitumika

kama kihusishi.

Yeye ni mrefu **kama** mlingoti.

Kama ni kihusishi cha kulinganisha.

## VITENZI

Vitenzi ni maneno ambayo hudhihirisha jinsi kitendo kilivyofanywa, kinavyofanyika au kitakavyofanyika.

Maswali kuhusu vitenzi katika mitihani yatachukua mitindo ifuatayo.

**Mtindo wa kwanza**

**Swali la KCSE 2014**

Ainisha vitenzi katika sentensi:

Ndege yu taabani, hata hivyo anajaribu kujinasua.

yu – kitenzi kishirikishi

anajaribu ni kitenzi kisaidizi

kujinasua ni kitenzi kikuu

**Mtindo wa pili**

**Swali la KCSE 2013**

Tunga sentensi yenye kikundi tenzi chenye muundo ufuatao:

kitenzi kisaidizi, kitenzi kikuu, nomino

Wachezaji walikuwa wanapiga mpira.

walikuwa- kitenzi kisaidizi

wanapiga – kitenzi kikuu

mpira – nomino

**Aina za vitenzi**

**(a) Vitenzi vikuu**

Hivi ni vitenzi ambavyo huwasilisha maana bila ya kutegemea viambishi au maneno mengine.

Baadhi ya vitenzi hivi ni nasua, piga, lima, cheza, panda na soma.

**Mifano katika sentensi**

Watoto **wanacheza** uwanjani.

Wakulima **wanalima** shambani.

**(b) Vitenzi halisi**

Ni vitenzi ambavyo hutegemea viambishi ili kuwasilisha maana.

Baadhi ya vitenzi hivi ni waliwatembelea, wanakuja, alimjongelea na tuliongelea.

Wote wanakuja kesho.

Wazazi wake waliwatembelea watoto mayatima.

**(c) Vitenzi visaidizi**

Vitenzi hivi hufanya kazi ya kusaidia vitenzi halisi na vitenzi vikuu. Vitenzi hivi haviwezi kutokea peke yake katika sentensi.

**Mifano ya vitenzi hivi ni** kuwa, jaribu, wahi, enda, pata, taka na pasa.

Vitenzi visaidizi ni rahisi kuvitambua kwani ni lazima vishirikiane na vitenzi vingine ili kutoa maana katika sentensi.

Mgonjwa alikuwa ametembelewa na jamaa zake.

**alikuwa** ni kitenzi kisaidizi

**ametembelewa** ni kitenzi halisi

**(d) Vitenzi vishirikishi**

Kuna vitenzi vishirikishi vipungufu na vitenzi vishirikishi vikamilifu.

**(i) Vitenzi vishirikishi vipungufu**

Vitenzi hivi havichukui viambishi na hivyo vinafahamika kama vitenzi vishirikishi vipungufu.

**Mifano ni** u, ni, ki, m, li na si.

Tunda li mtini.

Kitabu ki mezani.

**(ii) Vitenzi vishirikishi vikamilifu**

Vitenzi hivi huchukua viambishi mbalimbali. Baadhi ya vitenzi hivi ni ngali, ndiye, lipo na wamo.

**Mfano katika sentensi**

Mama angali sokoni.

**(e) Vitenzi sambamba**

Muundo wake ni wa vitenzi viwili au zaidi ambavyo vinafuatana.

**Mifano**

Watoto **walikuwa wanacheza** uwanjani

vitenzi sambamba

Mimea **iliweza kukauka kutokana** na ukame.

Vitenzi sambamba hushirikisha kitenzi kisaidizi na kitenzi kikuu au kitenzi kisaidizi na kitenzi halisi.

**Swali la KCSE 2008**

Tambua aina ya kitenzi kilichopigwa mstari katika sentensi.

Mzee **huenda** anacheza kamari.

huenda – kitenzi kisaidizi

**Swali la KCSE 2012**

Tunga sentensi yenye kitenzi kishirikishi kikamilifu.

Mazao **yangali** shambani.

## VIVUMISHI

Haya ni maneo ambayo hutoa taarifa zaidi kuhusu nomino. Aghalabu nafasi ya vivumishi katika sentensi ni baada ya nomino.

**Mifano**

Mtoto mdogo anakunywa maziwa.

**mdogo** ni kivumishi

Mwanamke mrembo ameshiriki katika mashindano ya uzuri.

**mrembo** ni kivumishi

Hata hivyo si lazima vivumishi vifuate nomino. **Mifano,**

Jambazi lililouliwa ni hatari.

hatari ni kivumishi

Mtoto huyu ni mtundu.

mtundu ni kivumishi

Kuna mitindo miwili ya kutahini mada hii,

### Mtindo wa kwanza

Tunga sentensi ukitumia kivumishi cha pekee chenye kuleta dhana ya bila kubagua.

Simu **yoyote** itatumiwa.

**Mtindo wa pili**

**Swali la KCSE 2010**

Tambua na ueleze aina za vivumishi katika sentensi:

Mwanafunzi mkongwe amepewa tuzo kwa kuwa hodari masomoni.

Mkongwe na hodari ni vivumishi vya sifa.

**Aina za vivumishi**

**(a) Vivumishi vya sifa**

Ni vivumishi ambavyo vinatoa taarifa kuhusu nomino kwa kueleza sifa za nomino hiyo.

**Mifano ni** hodari, mkongwe, mrembo, mfupi, sugu, mvivu, mlafi na jasiri.

**Mifano katika sentensi**

Mwanariadha **hodari** amepokea tuzo.

Msichana **mkakamavu** anawasaidia watoto mayatima.

**(b) Vivumishi vya kumiliki (vivumishi vimilikishi)**

Vivumishi hivi huonyesha vitu vinavyorejelewa ni vya nani. Jedwali lifuatalo linaonyesha vivumishi vimilikishi.

| Nafsi | Umoja | Wingi |
|---|---|---|
| kwanza | -angu | -etu |
| pili | -ako | -enu |
| tatu | -ake | -ao |

Daftari **langu** limesahihishwa.

Madaftari **yetu** yamesahihishwa.

Kisu **chako** kilinolewa.

Visu **vyenu** vilinolewa.

Saa **yake** iliharibika.

Saa **zao** ziliharibika.

**(c) Vivumishi vya idadi**

Ni vivumishi ambavyo hutoa taarifa zaidi kuhusu nomino kwa kuonyesha idadi inayohusika. Vivumishi hivi ni vya aina mbili; vya idadi halisi na vya idadi ya jumla.

**(i) Vivumishi vya idadi ya jumla**

Hivi havibainishi idadi kamili inayohusika.

Mifano,

Watalii **wachache** wamewasili nchini.

Mifugo **wengi** wamechanjwa.

**(ii) Vivumishi vya idadi kamili**

Huonyesha idadi halisi inayohusiana na nomino inayovumishwa.

**Mifano**

Mikeka **mitatu** itatumiwa na waumini.

Taa **kumi** za umeme zitahitajika.

**(d) Vivumishi viulizi**

Ni vivumishi vinavyofanya dhima ya kudadisi. Hivi ni –ngapi, -pi na gani.

**Mifano katika sentensi**

Kondoo **yupi** atachinjwa?

Magari **mangapi** yamepata ajali?

Milango **gani** itakarabatiwa?

Kivumishi kiulizi gani hakichukui viambishi vyovyote. Sentensi ifuatayo si sahihi.

*Milango migani itakarabatiwa? si sahihi

Milango gani itakarabatiwa? sahihi

**(e) Vivumishi vionyeshi/ vivumishi viashiria**

Hufanya kazi ya kuonyesha umbali wa nomino inayorejelewa. Kuna vya karibu, vya mbali kidogo au vya mbali sana.

Hutegemea ngeli inayorejelewa.

**Mifano,** hiki hicho kile

huyu huyo yule

hili hilo lile

huu huo ule

hapa hapo pale

**Mifano katika sentensi**

Mdudu **huyu** ni hatari.

Wadudu **hawa** ni hatari.

Mahali **hapo** panapendeza.

Ufunguo **ule** hautumiki.

Funguo **zile** hazitumiki.

**(f) Vivumishi vya pekee**

Vivumishi hivi ni –ote, -o-ote, -enye, –enyewe, –ingine na –ingineo.

(i) **-ote**

Huleta dhana ya kutobakiza. Huongezwa viambishi kwa kutegemea ngeli.

Ukuta **wote** umepakwa rangi.

Vikombe **vyote** vitatumiwa.

(ii**) -o-ote**

Hivi huonyesha wazo la kutobagua.

Mfanyakazi **yeyote** atapewa cheti.

Ubao **wowote** utatumiwa.

(iii) **-enye**

Huibua dhana ya kuhodhi kitu.

Daktari **mwenye** kliniki amekamatwa.

Chumba **chenye** dawa kitafungwa.

(iv) **-enyewe**

Huleta dhana ya msisitizo.

Kibuyu **chenyewe** kilitoboka.

Msafiri **mwenyewe** alighushi hati.

(e) **-ingine**

Kivumishi cha pekee – ingine huleta dhana ya nyongeza.

Kiti **kingine** kitatumika.

Jembe **lingine** litanunuliwa.

**(g) Vivumishi vya nomino**

Hudhihirika wakati nomino mbili zinafuatana. Katika hali hiyo, nomino ya pili hubadilika na kuwa kivumishi cha nomino.

Dereva **msichana** ameepuka ajali.

msichana ni kivumishi cha nomino

Mwalimu **kijana** aliandika mashairi.

kijana ni kivumishi cha nomino

**(h) Vivumishi virejeshi**

Hivi hutoa taarifa zaidi kuhusu nomino kwa kuirejelea. Vivumishi hivi ni vya aina mbili:

(i) 'O' rejeshi

'O' rejeshi huchopekwa kwenye vitenzi.

Kuna 'o' rejeshi tamati na 'o' rejeshi kati.

**Mifano**

Nyota zili**zo**ng'aa zilikiondoa kiza.

Ngamia ali**ye**umia ni yule.

(ii) Kirejeshi amba

Huchukua viambishi kwa kutegemea ngeli.

Harusi **ambayo** ilifanyika ni ya waziri.

Ufunguo **ambao** ulipotea umepatikana.

Vivumishi ‘o’ rejeshi na amba- haviwezi vikatumika pamoja katika sentensi. Sentensi ifuatayo si sahihi.

*Mkulima ambaye aliyepata mazao mengi ni yule.

Sentensi hii inaweza kusahihishwa kwa njia mbili.

1 Mkulima ambaye alipata mazao mengi ni yule.

2 Mkulima aliyepata mazao mengi ni yule.

**(i) Vivumishi vya ‘a’ unganifu**

‘a’ unganifu ni kivumishi cha uhusiano. Huwekwa viambishi kwa kutegemea ngeli.

Jembe **la** mkulima limetiwa makali.

Utawala **wa** kiimla haudumu.

Kisu **cha** mpishi ni kikali.

**Swali la KCSE 2013**

Tunga sentensi moja kubainisha:

Kivumishi cha pekee chenye maana, “bila kuchagua”.

Uzi **wowote** utatumiwa.

SWALI LA KCSE 2019

Tunga sentensi ukitumia vivumishi vinavyotoa maana zifuatazo:

(i) Nafasi katika orodha

Mwanariadha **wa** kwanza atapokea hela nyingi.

(ii) Kutobagua

Kalamu **yoyote** itatumiwa.

**(j) Vivumishi visisitizi**

Vivumishi visitizi hutoa taarifa zaidi kuhusu nomino kwa kuitilia mkazo. Vivumishi hivi aidha huonyesha umbali wa nomino inavyovumishwa.

**Mifano**

| NGELI | NOMINO | KARIBU | VYA MBALI KIDOGO | VYA MBALI SANA |
|---|---|---|---|---|
| A – WA | msafiri | yuyu<br>huyu | yuyo<br>huyo | yule<br>yule |
| U – ZI | uzi | uu<br>huu | uo<br>huo | ule<br>ule |
| LI – YA | jani | lili<br>hili | lilo<br>hilo | lile<br>lile |

**<u>VIWAKILISHI</u>**

Haya ni maneno ambayo hutumiwa ikiwa sentensi haina nomino. Sentensi ya Kiswahili haitakuwa na nomino au kiwakilishi cha nomino kwa wakati mmoja.

Mitindo ya utahini katika mada hii

**(i) Mtindo wa kwanza**

**Swali la KCSE 2011**

Tumia mzizi '-enye' katika sentensi kama:

(i) kiwakilishi

**Mwenye** shamba hilo ameondoka.

**(ii) Mtindo wa pili KCSE 2012**

Ainisha maneno yalipigiwa mstari.

**Naam**, ameleta **machache**.

machache ni kiwakilishi cha idadi ya jumla

**Aina za viwakilishi**

**(a) Viwakilishi viashiria/ vionyeshi**

Hubainisha umbali wa kitu.

Kuna viwakilishi viashiria vya karibu, vya mbali kidogo au vya mbali sana.

Mifano katika sentensi.

**Hiki** kina makali.

**Hilo** litatumiwa na mkulima.

**Yule** anaongoza jimbo visivyo.

**(b) Viwakilishi vya pekee**

Hutokana na mzizi –ote, -o-ote, –enye, -enyewe, -ingine na -ingineo. Huwekwa viambishi kwa kutegemea ngeli.

**Chote** kimeliwa.

**Lolote** litatumiwa na mwashi.

**Mwingine** umeleta maafa nchini.

**Mwenyewe** atapokea zawadi tele.

**(c) Viwakilishi vya sifa**

Ni maneno ambayo hutoa sifa. Mifano ya viwakilishi vya sifa ni mkongwe, dhaifu, kirefu, mwerevu, hodari, mtundu na sugu.

**Mifano katika sentensi**

**Mtundu** atapokea ushauri nasaha.

**Kikali** kitatumiwa na wapishi.

**(d) Viwakilishi vya idadi**

Ni maneno yanayosimama mahali pa nomino yakiwa yanaonyesha idadi ya watu au vitu vinavyohusika. Kuna viwakilishi vya idadi halisi na vya idadi ya jumla.

**(i) Viwakilishi vya idadi halisi**

Huonyesha idadi kamili ya vitu au watu wanaorejelewa.

**Mifano katika sentensi**

**Watatu** wamekwenda mjini.

**Vinne** vitatumiwa na wageni.

**(ii) Viwakilishi vya idadi ya jumla**

Ni maneno ambayo hayaonyeshi idadi halisi.

**Mifano katika sentensi**

**Wengi** walipokea chanjo dhidi ya ugonjwa huo.

**Machache** yamepoteza makali.

**(e) Viwakilishi vimilikishi**

Hufanya kazi ya kuonyesha umiliki.

| Nafsi | umoja | wingi |
|---|---|---|
| kwanza | -angu | -etu |
| pili | -ako | -enu |
| tatu | -ake | -ao |

**Yangu** itatumika jioni.

**Lenu** linataka ukarabati.

**Chake** kilikuwa na dosari.

**(f) Viwakilishi viulizi**

Viwakilishi viulizi ni maneno yanayofanya dhima ya kuuliza. Mizizi ya viwakilishi viulizi ni – ngapi, - pi na gani.

**Mifano katika sentensi**

**Gani** litatumiwa shambani?

**Upi** ulitumiwa kufungua kufuli?

**Wangapi** waliingia nchini?

**(g) Viwakilishi virejeshi**

Viwakilishi virejeshi ni vya aina mbili, 'o' rejeshi na kirejeshi ' amba'. Viwakilishi hivi hutegemea ngeli inayorejelewa.

**Ambaye** ni mvivu atapata matokeo duni.

**Ambayo** imepokelewa ina utata.

Zili**zo**bomoka zitazibwa.

**(h) Viwakilishi vya 'a' unganifu**

Hukitwa kwenye mzizi 'a' kwa kutegemea ngeli.

**Mfano**

**Wa** kisukari unawaathiri watu walio na umri mkubwa.

**(i) Viwakilishi visisitizi**

Hufanya kazi ya kusisitiza. Hutegemea ngeli inayowakilishwa.

**Mifano katika sentensi**

**Kuku huku** kunapendeza sana.

**Yale yale** yana kemikali hatari.

**Swali la KCSE 2013**

Tumia kiwakilishi cha 'a' unganifu katika sentensi kuonyesha:

(i) Umilikaji

(ii) nafasi katika orodha au nafasi katika kundi

**Wa** Rashid umebeba vitu vingi.

**Wa** kwanza katika mbio hizo atapokea hela nyingi.

## VIELEZI

Vielezi ni maneno ambayo yanafanya kazi ya kutoa taarifa zaidi kuhusu vitenzi, vivumishi au vielezi vingine.

**Aina za vielezi**

**(a) Vielezi vya mahali**

Hubainisha au hudokeza dhana ya mahali ama mahali kitendo kinapo-tendeka.

**Mifano katika sentensi**

Mgonjwa yumo **hospitalini**.

Vielezi hujibu swali **wapi**?

Wamekwenda **Mombasa**.

Daftari limeanguka **sakafuni**.

Ndege amepaa **juu**.

Panya ameingia **humo**.

**(b) Vielezi vya wakati**

Hudhihirisha wakati kitendo kinapotokea.

Mzee alikwenda **Jumamosi**.

Mizigo ilipokelewa **jioni**.

Vielezi vya wakati hujibu swali **lini**?

Mifano ya vielezi vya wakati ni vile vinavyoonyesha siku za juma, miezi, misimu mbalimbali au nyakati mbalimbali.

Mtihani wa kitaifa utatangazwa **Mei**.

Alirina asali **saa mbili usiku**.

**(c) Vielezi vya namna/jinsi**

Huonyesha namna au jinsi kitendo kilivyofanyika au kitakavyofanyika. Vielezi hivi hujibu swali **vipi**.

**Aina za vielezi vya namna**

**(i) Vielezi vya namna vikariri**

Musechi anaongea **harakaharaka**.

Siafu hao wanatembea **polepole**.

**(ii) Vielezi vya namna viigizi**

Hutokana na kuiga mlio wa kitu kinachotendeka. **Mifano ni:** chubwi, tifu, kwakwakwa na fofofo.

**Mifano katika sentensi**

Alianguka mchangani **tifu**.

Baada ya safari ndefu, walilala **fofofo**.

**(iii) Vielezi vya namna hali**

Vielezi vya namna hali hudhihirisha hali ya kutokea kwa kitendo kwa kurejelea kinachohusika katika kufanya kitendo hicho.

Walifanya mazoezi hayo **kwa bidii**.

Polisi waliwasili **kwa vishindo** katika eneo la mkasa.

**(iv) Vielezi vya namna halisi**

Hivi hutumia maneno halisi yanayoonyesha namna kitendo kili-vyotukia au kilivyofanyika.

Ng’ombe walipelekwa malishoni **haraka** na mchungaji.

Bidhaa zilitengenezwa **upesi**.

**(v) Vielezi vya namna ala au kitumizi**

Huonyesha kifaa kilichotumiwa katika kutekeleza kazi fulani.

Walisafiri kwa **basi**.

Nyumba ilijengwa kwa **mbao**.

**(vi) Vielezi vya namna mfanano**

Huundwa kwa kuongeza kiambishi **ki** kwenye mizizi ya maneno ili kudhihirisha jinsi kitendo kinavyotendeka.

Washiriki wa mashindano ya uzuri walitembea **kitausi**.

Aliukabili umati huo **kishujaa** alipohimizwa atoe hotuba.

**(d) Vielezi vya idadi**

Hivi ni vielezi ambavyo huonyesha kitendo kinatukia mara ngapi. Vielezi hivi hujibu swali **mara ngapi** au **kwa kiasi** gani.

Kuna vielezi vya idadi ya jumla na vielezi vya idadi halisi.

**(i) Vielezi vya idadi halisi**

Hudhihirisha kitendo kinatokea mara ngapi kwa kuonyesha idadi kamili.

Madaftari hayo yalisahihishwa **mara tatu**.

Ng'ombe walinyweshwa maji **mara mbili** na mfungaji.

**(ii) Vielezi vya idadi ya jumla**

Hivi huonyesha idadi isiyo kamili ya kutokea kwa kitendo.

Miche ilipandwa **mara chache** na wakulima.

Ugonjwa huo ulipotokea, mikutano ya kutafuta ufumbuzi ilifanyika **mara nyingi**.

**Swali la KCSE 2000**

Taja vielezi vinavyopatikana katika sentensi hizi

(i) Aliamka **alfajiri**.

cha wakati

(ii) Mtu huyu ni hodari **sana**.

kielezi cha namna halisi

**SWALI LA KCSE 2004**

Tambulisha kielezi, kivumishi na mnyambuliko wa kitenzi katika sentensi ifuatayo.

Msichana mrembo alikuja **upesi** akikimbilia dadake.

kielezi cha namna halisi

**Swali la KCSE 2006**

Tunga sentensi ukitumia kielezi cha:

(i) wakati (ii) mahali

Nyuki walifukuzwa **mzingani**.

kielezi cha mahali

Mkutano unatarajiwa kuanza **alasiri**.

kielezi cha wakati

## VIHISISHI

Haya ni maneno ambayo huonyesha hisia tofautitofauti kama kukubali, huzuni, maumivu, mshangao, furaha, huruma au hofu.

Baada ya kihisishi, herufi kubwa hutumiwa.

**Mfano**

Do! Kiongozi huyo amehusika katika ufisadi.

### Aina za vihisishi

**(i) Vihisishi vya furaha**

Huleta hisia za furaha.

Baadhi ya vihisishi hivi ni hoyee, hongera, huree, mashallah na hario.

**Mifano katika sentensi**

**Oyee**! Timu yetu imeshinda.

**(ii) Vihisishi vya mshangao**

Hubainisha hali ya kushangazwa na kitendo kilichotokea.

**Lo**! Mzee huyo ni mwizi.

**Salalee**! Nyuki hao wamemuua ndovu.

Mifano zaidi ya vihisishi hivi ni do, ala, masalaale na salalaa,

**(iii) Vihisishi vya kukataa**

Ni vihisishi vinavyoleta dhana ya kutoafikiana na hali fulani.

**La**! Uamuzi huo utawaponza watu wote.

Mifano zaidi ya vihisishi hivi ni **hasha, hata**, n.k.

**(iv) Vihisishi ya huzuni**

Huonyesha hisia za masikitiko.

**Mifano,** maskini, mtume na mama we.

**Maskini**! Sijui kama atanusurika na mkasa huo.

**SWALI LA KCSE 2015**

Tunatumia kihisishi "makiwa" tunapotoka kumtuliza aliyefiwa, na …. ……….tunapotaka mtu atupishe.

Jawabu ni hebu, simile au hela.

**(v) Vihisishi vya kuapa**

Hutumika katika miktadha ambapo watu wanaahidi kutekeleza jambo fulani.

**Mifano,** wallahi na haki ya Mungu.

**Wallahi**! Nitakupa hela zote ulizonikopesha.

**(vi) Vihisishi vya kuitikia**

Hutumika katika miktadha ya mazungumzo unapomhimiza mtu aendelee kuzungumza au kuafikiana na kauli iliyotolewa.

**Mifano ni** ehee, enhee, naam na taib.

**Taib**! Maelezo yako yanashabihiana na kauli iliyotolewa mwaka uliopita.

**(vii) Vihisishi vya dharau**

Hivi ni vihisishi vya kubeza au kuonyesha hali ya kutoheshimu.

Baadhi ya vihisishi ni ebo, kefule, po, aka na he.

**Ebo**! Mtoto anawavunjia heshima wazazi wake.

**Po**! Huyu hana maarifa kuhusu suala hili.

**Swali la KCSE 2012**

Ainisha maneno yaliyopigiwa mstari.

**Naam**, ameleta machache.

Naam ni kihisishi cha kuitikia.

Maswali katika mada hii yanaweza yakatokea katika njia zifuatazo:

(1) Bainisha aina za vihisishi katika sentensi zifuatazo.

**Lo**! Ng'ombe dume amemuua chui.

kihisishi cha mshangao

**Hoyee**! Nimepita mtihani uliokuwa mgumu.

kihisishi cha furaha

(2) Tunga sentensi ukitumia:

(i) kihisishi cha kuapa

(ii) kihisishi cha kuitikia

## KIIMA NA KIARIFA

Hii ni sehemu katika sentensi ambayo hujumuisha nomino pekee au nomino na maneno mengine bila ya kitenzi. Hushirikisha vilevile kiwakilishi pekee au kiwakilishi na maneno mengine.

**Mifano**

**Mtoto** amelia sana.

kiima

**Mwenyewe** ameondoka.

kiima

**Msichana mrembo** anasoma chuoni.

kiima

**Asha, kiptoo na Mary** ni jasiri.

kiima

**Swali la KCSE 2012**

Bainisha kiima na chagizo katika sentensi ifuatayo

Watahiniwa hao walisoma maswali yote kwa makini.

kiima ni **watahiniwa hao**

## KIARIFA

Ni sehemu katika sentensi ambayo ina kitenzi au kitenzi na maneno mengine.

Mvua **ilinyesha**.

kiarifa

Mvua **ilinyesha sana**.

kiarifa

Maswali kuhusu mada hii yanaweza yakatokea katika mitindo miwili:

### Mtindo wa kwanza

(1) Eleza maana ya dhana zifuatazo:

(i) kiima

(ii) kiarifa

### Mtindo wa pili

(2) Bainisha kiima na kiarifu katika sentensi ifuatayo.

Mifereji yote imekarabatiwa.

**mifereji yote** ni **kiima**

**imekarabatiwa** ni **kiarifa**

## SHAMIRISHO/ YAMBWA NA CHAGIZO

### Chagizo

Ni neno au maneno ambayo yanafanya kazi ya vielezi.

**Mifano**

Tutawapa zawadi **kesho jioni**.

chagizo

Mimea hiyo ilikomaa **haraka.**

chagizo

## SHAMIRISHO /YAMBWA

Shamirisho ni neno ambalo hubainisha mtendwa au mtendewa katika sentensi.

Zipo aina tatu kuu za shamirisho.

### (a) Shamirisho kitondo

Ni mtu au kitu ambacho kinapokea kitendo ambacho kinatekelezwa.

**Mifano**

Mogaka alimpikia **mkewe** chakula.

Mkewe ni shamirisho kitondo kwa kuwa hiyo ndiyo nomino inayopokea kitendo.

Babu alimzawidi **mjukuu** wake.

Mjukuu ni shamirisho kitondo.

Shamirisho kitondo pia hujulikana kama **yambwa tendewa** au **yambiwa**

### (b) Shamirisho kipozi

Shamirisho kipozi hurejelea kitu ambacho kinaathiriwa na kitendo kinachoangaziwa.

Mzee yule amenunua **taa**.

taa ni shamirisho kipozi

Shamirisho kipozi aidha hujulikana kama **yambwa tendwa**.

**Swali la KCSE 2014**

Andika upya sentensi ifuatayo ukianza kwa yambwa tendwa.

Wafugaji waliwakatia ng'ombe wote majani ya mti huo.

Majani ya mti huo yalikatiwa ng'ombe wote na wafugaji.

**(c) Shamirisho ala/ kitumizi**

Kitu kinachotumiwa kufanyia kitendo fulani hujulikana kama shamirisho ala.

**Mifano**

Alikwenda mjini kwa **basi.**

shamirisho ala

Nyumba yake imejengwa kwa **mawe**.

shamirisho ala

Mitindo ya kutahini mada hii,

**Mtindo wa kwanza**

Bainisha aina za shamirisho katika sentensi hii.

Auma alimlipia nauli mamake na akasafiri kwa ndege.

**nauli** ni **shamirisho kipozi**

**mama** ni **shamirisho kitondo**

**ndege** ni **shamirisho ala**

**Mtindo wa pili**

Tunga sentensi iliyo na shamirisho kipozi na shamirisho kitondo.

**Mtindo wa tatu**

Bainisha yambiwa na yambwa tendwa katika sentensi ifuatayo.

Suleimani alimpa mwanawe kalamu.

**mwanawe** ni **yambiwa**

**kalamu** ni **yambwa tendwa**

**Swali la KCSE 2017**

Ainisha yambwa katika sentensi ifuatayo.( alama 2)

Mhunzi alimfulia mjukuu wake pete ya shaba.

**mjukuu** ni **yambiwa/yambwa tendewa**

**pete** ni **yambwa tendwa**

**Swali la KCSE 2015**

Bainisha kiima na chagizo katika sentensi ifuatayo:

Mwenyewe alikipenda kwa dhati.

kwa dhati ni chagizo

**Swali la KCSE 2010**

Ainisha shamirisho na chagizo katika sentensi .

Vibarua wamefanya kazi haraka ipasavyo.

**kazi** ni **shamirisho kipozi**

**Swali la KCSE 2011**

Onyesha shamirisho kitondo, kipozi na ala katika sentensi ifuatayo:

Kipkemboi alimbebea mwalimu mzigo kwa gari.

**mwalimu** ni **shamirisho kitondo**

**mzigo** ni **shamirisho kipozi**

**gari** ni **shamirisho ala**

**KCSE 2008**

Taja aina ya yambwa iliyopigiwa mstari sentensi ifuatayo:

Mpishi amempikia mgeni wali vizuri.

wali ni yambwa tendwa

## AINA ZA SENTENSI

Kuna aina tatu za sentensi. Nazo ni sentensi sahili, sentensi changamano na sentensi ambatano.

### Sentensi sahili

Hii ni sentensi ambayo huwasilisha wazo moja.

**Mifano ya sentensi sahili**

Mkulima mzembe amepata hasara.

Mvulana mrefu anavuka barabara.

**Sentensi ambatano**

Ni sentensi mbili sahili au zaidi zilizounganishwa kwa kutumia kiunganishi.

**Mifano,**

Watalii wanatazama wanyama lakini dereva anaendesha gari.

Shujaa alipata zawadi nyingi kwa kuwa alilikomboa taifa lake.

Mchezo umemalizika na mashabiki wanawapigia wachezaji makofi.

**Swali la KCSE 2006**

Sentensi hizi ni za aina gani?

1. **Lonare anatembea kwa kasi**.

Hii ni sentensi sahili.

2. **Halima anaandika hali Ekomwa anasoma**.

Ni sentensi ambatano

**Swali la KCSE 2008**

Tumia mfano mmoja mmoja kutofautisha baina ya sentensi sahili na ambatano.

Abiria walisafiri kwa ndege. **sahili**

Mama anasoma gazeti lakini baba anatazama televisheni. **Ambatano**

**Sentensi changamano**

Sentensi iliyo na kishazi huru pamoja na kishazi tegemezi hutambulika kama sentensi changamano.

**Mifano**

Gari lililokarabatiwa jana limebeba abiria.

Gari limebeba abiria. **kishazi huru**

lililokarabatiwa jana **kishazi tegemezi**

Nzige ambao ni hatari wameharibu mimea.

Nzige wameharibu mimea. **kishazi huru**

ambao ni hatari **kishazi tegemezi**

Madaftari yalisahihishwa tulipokuwa darasani.

Madaftari yalisahihishwa. **kishazi huru**

tulipokuwa darasani **kishazi tegemezi**

Licha ya kwamba wagonjwa waliteseka, wauguzi waliendelea na mgomo.

**kishazi tegemezi** **kishazi huru**

**Swali la KCSE 2012**

Huku ukitoa mfano, eleza maana ya sentensi changamano.

**Swali la KCSE 2018**

Maji yalijaa. Maji yalimwagika.

(Unganisha kuunda sentensi changamano.)

Maji yaliyojaa yalimwagika.

**Swali la KCSE 2019**

Vyakula viliandaliwa. Vyakula vilikuwa na viinilishe muhimu.

(unganisha kuunda sentensi changamano)

Vyakula vilivyoandaliwa vilikuwa na viinilishe muhimu.

## VISHAZI

Kishazi ni kifungu cha maneno ambacho kina muundo wa kiima na kiarifa. Katika sentensi kuna aina mbili kuu za vishazi; kishazi huru na kishazi tegemezi.

### Vishazi huru

Hivi ni vishazi ambavyo huwasilisha maana bila kutegemea vishazi vingine. Vishazi hivi hujitosheleza kimaana na huweza kujitokeza kama sentensi kamili.

**Mifano katika sentensi**

Fatuma aliyesafiri kijijini alilakiwa na wazee wake.

**kishazi huru**

Fatuma alilakiwa na wazee wake.

Ziwa ambalo limejaa maji lina samaki wengi.

**kishazi huru**

Ziwa lina samaki wengi.

Mihogo iliharibiwa tulipokuwa shambani.

**kishazi huru**

Mihogo iliharibiwa.

**Vishazi tegemezi**

Vishazi tegemezi havijitoshelezi kimaana. Hutegemea vishazi huru ili kuwasilisha maana kamili. Vishazi hivi vinaweza vikaondolewa katika sentensi na sentensi husika ikadumisha maana. Ina maana kwamba, vishazi tegemezi vitawasilisha maana endapo vitaambatana na vishazi huru.

**Vishazi hivi hudhihirika katika sentensi kwa kuwepo kwa 'o' rejeshi**.

**Mfano**

Mitambo iliyoharibiwa jana ilikuwa inatumiwa na magaidi.

iliyoharibiwa jana ni kishazi **tegemezi**

Mvua ilinyesha tulipokuwa kijijini.

tulipokuwa kijijini ni **kishazi tegemezi**

**Aidha baadhi ya viunganishi hudokeza kuwepo kwa vishazi tegemezi**.

Hata ingawa mvua ilinyesha, mimea mingi ilikauka.

hata ingawa mvua ilinyesha ni **kishazi tegemezi**.

Ingawa mshahara wake si mkubwa anaikimu familia yake.

ingawa mshahara wake si mkubwa **kishazi tegemezi**

Anaikimu familia yake. **kishazi huru**

**Swali la KCSE 2017**

Ainisha vishazi katika sentensi ifuatayo:

Viwanda vikianzishwa mashambani idadi ya wanaohamia mjini

itapunguzwa.

viwanda vikianzishwa mashambani **kishazi tegemezi**

Idadi ya wanaohamia mjini itapunguzwa. **kishazi huru**

**Swali la KCSE 2013**

Ainisha vishazi katika sentensi ifuatayo.

Ingawa mshahara wake si mkubwa anaikimu familia yake.

ingawa mshahara wake si mkubwa **kishazi tegemezi**

anaikimu familia yake. **kishazi huru**

**Swali la KCSE 2007**

Bainisha kishazi huru na kishazi tegemezi katika sentensi ifuatayo:

Mkulima aliyepanda wakati ufaao amepata mavuno mazuri.

aliyepanda wakati ufaao **kishazi tegemezi**

Mkulima amepata mavuno mazuri. **kishazi huru**

**Swali la KCSE 2019**

Ainisha vishazi katika sentensi ifuatayo.

Usalama ukiimarishwa watalii wengi watakuwa wanazuru humu.

usalama ukiimarishwa **kishazi tegemezi**

Watalii wengi watakuwa wanazuru humu. **kishazi huru**

Mitindo ya kutahini mada hii

**Mtindo wa kwanza**

Tunga sentensi iliyo na kishazi tegemezi.

**Mtindo wa pili**

Ainisha vishazi katika sentensi ifuatayo:

Msumeno uliotumiwa na fundi umechakaa.

Msumeno umechakaa. kishazi huru

uliotumiwa na fundi kishazi tegemezi

## VIRAI

Kirai ni neno au kifungu cha maneno ambacho hakitoi taarifa kamili.

**Aina za virai**

**(a) Kirai nomino**

Muundo wa kirai nomino umekitwa kwenye nomino pekee au nomino na maneno mengine au kiwakilishi pekee au kiwakilishi na maneno mengine.

**Mifano ya virai nomino katika sentensi**

**Baiskeli** imenunuliwa.
kirai nomino

**Abdi, Omari na Zuena** ni watundu.
kirai nomino

**Jambazi sugu** limeuliwa.
kirai nomino

**Yule** ni hodari.
kirai nomino

**Hawa warefu** wanacheza vizuri.
kirai nomino

Neno kuu linalotawala katika kirai nomino ni nomino au kiwakilishi cha nomino.

**(b) Kirai kitenzi**

Katika kirai kitenzi, neno kuu ni kitenzi. Kirai kitenzi huundwa na kitenzi pekee au kitenzi na maneno mengine.

**Mifano ya sentensi zilizo na virai vitenzi**

Maji **yamemwagika**.
kirai kitenzi

Mkeka **uliochafuka umenadhifishwa**.
kirai kitenzi

Wazee **waliwatembelea mjini**.
kirai kitenzi

**(c) Kirai kivumishi**

Kirai kivumishi ni kirai ambacho neno linalotangulia ni kivumishi. Neno kuu katika kirai kivumishi ni kivumishi.

**Mifano katika sentensi**

Mwanafunzi **mrefu sana** ameondoka.

kirai kivumishi

Mdudu **mdogo mweusi** amemng'ata.

kirai kivumishi

**(d) Kirai kielezi**

Katika kirai kielezi, neno linalotangulia huwa ni kielezi. Neno kuu katika kirai kielezi ni kielezi.

**Mifano katika sentensi**

Aliadhibiwa **vibaya sana**.

kirai kielezi

Mti ulianguka **mtoni jana jioni**.

kirai kielezi

**(e) Kirai kiunganishi**

Neno kuu katika kirai kiunganishi ni kiunganishi. Kirai kiunganishi hutangulizwa na kiunganishi.

**Mifano katika sentensi**

Shule zilifungwa **kwa sababu ya mgomo**.

kirai kiunganishi

Kirai kiunganishi huundwa kwa kuwepo kwa kiunganishi.

**(f) Kirai kihusishi**

Huundwa kwa vihusishi mbalimbali. Neno linalotangulia kirai kihusishi ni kihusishi.

Mtungi **wa mama** umetoboka.

kirai kihusishi

Mwavuli umewekwa **chini ya meza**.

kirai kihusishi

**Swali la KCSE 2018**

Ainisha virai katika sentensi ifuatayo.

Viongozi wengi walikuwa waadilifu mno kabla ya uchaguzi mkuu.

viongozi wengi **kirai nomino**

walikuwa waadilifu mno **kirai kitenzi**

kabla ya uchaguzi mkuu **kirai kihusishi**

**Swali la KCSE 2006**

Bainisha kirai nomino na kirai kitenzi katika sentensi .

Jirani mwema alinipa chakula.

jirani mwema **kirai nomino**

alinipa chakula **kirai kitenzi**

**Swali la KCSE 2015**

Tunga sentensi yenye muundo ufuatao. Nomino ya jamii, kirai kihusishi, kitenzi kishirikishi, kielezi cha mahali.

Umati wa watu mbele ya jukwaa ungali shereheni.

**Swali la KCSE 2014**

Ainisha virai vilivyopigwa mstari.

Zana hizi zimeundwa na mafundi wenye ustadi mkubwa.

na mafundi **kirai kihusishi**

wenye ustadi mkubwa **kirai kivumishi**

**Swali la KCSE 2012**

Bainisha aina za virai vilivyopigiwa mstari.

Ubaguzi wa kijinsia umekashifiwa na viongozi wenye msimamo thabiti mno.

wa kijinsia **kirai kihusishi**

viongozi wenye misimamo thabiti mno **kirai nomino**

**Maswali kuhusu virai hutokea katika njia zifuatazo**.

1 Eleza maana ya kirai.

2 Tunga sentensi ukitumia kirai kielezi na kirai nomino.

3 Bainisha virai katika sentensi ifuatayo.

Vitabu hivi vilitumiwa jana.

vitabu hivi **kirai nomino**

vilitumiwa jana **kirai kitenzi**

## MWINGILIANO WA MANENO

Ni hali ambapo neno moja linaweza kuwa na matumizi mbali-mbali.

Maneno mbalimbali yanakuwa na matumizi tofautitofauti.

**Mfano**

1. Mtoto huyu ni jasiri.

Neno **huyu** limetumika kama kivumishi.

2. Huyu ni jasiri.

Neno **huyu** limetumika kama kiwakilishi.

Katika sentensi hizo mbili neno huyu linatumika kama kivumishi katika sentensi ya kwanza na kama kiwakilishi katika sentensi ya pili. Ina maana kwamba neno moja limekuwa na matumizi tofauti. Mwingiliano wa maneno hutokea katika viwango mbalimbali ambavyo ni:

**(a) Kivumishi kuwa kiwakilishi**

1. Kisu **kirefu** kina makali.

kivumishi

2. **Kirefu** kina makali.

kiwakilishi

Katika sentensi hizi, neno kirefu linatumika kama kivumishi katika hali moja na kama kiwakilishi katika hali nyingine.

**(b) Nomino kuwa kiunganishi**

Ni hali ambapo neno lililotumika kama nomino katika hali moja likatumika kama kiunganishi katika hali nyingine.

**Mpaka** wa Kenya na Uganda una walinzi wengi.

**nomino**

Alijitahidi **mpaka** akafaulu.

**kiunganishi**

**(c) Nomino kuwa kielezi**

Neno ambalo ni nomino linaweza likatumika kama kielezi.

**Nairobi** ni mji mkuu wa Kenya.

**nomino**

Walienda **Nairobi**.

**kielezi**

(d) Kielezi kuwa kiwakilishi

Katika mwingiliano huu, neno ambalo ni kielezi linaweza likatumika kama kiwakilishi katika hali nyingine.

**Mifano**

Wachezaji walicheza **vizuri**.

**kielezi**

**Vizuri** vitatumiwa kupamba viti.

**Kiwakilishi**

**(e) Kihisishi kuwa kivumishi**

Neno ambalo linatumika kama kihisishi linaweza likatumika kama kivumishi katika hali nyingine.

**Maskini**! Amempoteza mjomba aliyekuwa akimsaidia.

**kihisishi**

Watoto **maskini** walipokea msaada.

**kivumishi**

**(f) Kielezi kuwa nomino**

Ni hali ambapo neno ambalo ni kielezi hutumika kama nomino katika hali nyingine.

Walitembea **taratibu** wakielekea mjini.

**kielezi**

**Taratibu** yake imemnyima nafasi ya kushinda mbio hizo.

**nomino**

**(g) Kihusishi kuwa kielezi**

Walisimama **kando** ya jukwaa.

**kihusishi**

Wote wamekwenda **kando**.

**kielezi**

**(h) Kitenzi kuwa kivumishi**

Katika hali hii, neno ambalo ni kitenzi hubadilisha matumizi yake na kuwa kivumishi.

Ali**batili** mkataba huo kutokana na kunyanyaswa na waliohusika.

**kitenzi**

Taarifa **batili** hazifai kusambazwa na mtu yeyote.

**Kivumishi**

**Mitindo ya kutahini mada hii,**

**Mtindo wa kwanza**

Eleza matumizi tofauti ya neno **msichana** katika sentensi zifuatazo.

1. Mtoto msichana anafaa kutunzwa vizuri.
2. Msichana yule ni hodari.

Katika sentensi ya kwanza neno msichana limetumika kama **kivumishi**. Katika sentensi ya pili limetumika kama nomino.

**Mtindo wa pili**

Tunga sentensi ukitumia neno **hili** kama kivumishi na kama kiwakilishi.

Tunda **hili** ni tamu.

**kivumishi**

**<u>Hili</u>** litatumiwa na mkulima.

**kiwakilishi**

**Swali la KCSE 2015**

Tunga sentensi kuonyesha matumizi yafuatayo ya neno: kama

(i) kiunganishi

(ii) kihusishi

Atulo ni mrefu **kama** twiga.

**kihusishi**

Chakula kitaiva **kama** utachochea kuni.

**kiunganishi**

**SWALI LA KCSE 2011**

Tumia mzizi (- enye) katika sentensi kama:

(i) kivumishi

(ii) kiwakilishi

**Mwenye** shamba amefika.

**kiwakilishi**

Mgeni **mwenye** gari ni yule.

**Kivumishi**

## <u>VIUNGANISHI</u>

Kiunganishi ni neno au kifungu cha maneno kinachotekeleza wajibu wa kuunganisha mafungu ya maneno au sentensi.

### Aina za viunganishi

### (a) Viunganishi vya kinyume

Haya ni maneno ambayo huunganisha sentensi au vifungu vya maneno kwa kuonyesha kinyume.

Mifano ya viunganishi vya kinyume ni lakini, ila, isipokuwa, walakini na bali.

**Mifano katika sentensi**

Alikuja **lakini** hakumwona.

Tulijitahidi **ila** hatukufanikiwa.

**(b) Viunganishi vya uteuzi**

Ni viunganishi ambavyo ni vya kuchagua kati ya vitu vilivyotolewa.

Mifano ya viunganishi hivi ni **au** na **ama.**

Maziwa yalimwagika au yalinywewa?

**(c) Viunganishi vya sababu**

Hivi huonyesha sababu ya kutukia kwa jambo fulani. Mifano ya viunganishi hivi ni ili, kwa sababu na kwa ajili.

Wanafunzi walitahiniwa ili kuchunguza kama walielewa mada hiyo.

Jengo lilibomolewa kwa sababu lilikuwa hatari kwa usalama wa wananchi.

**(d) Viunganishi vya masharti**

Huonyesha kuwa kutokea kwa jambo fulani kunaambatana na kutokea kwa jambo lingine

Mifano ni kama, endapo, iwapo, ikiwa, pindi na taraa.

**Mifano katika sentensi**

Shule zitafunguliwa kama kiwango cha maambukizi kitapungua.

Viatu vitadumu ikiwa vitapakwa rangi.

**(e) Viunganishi vya kuongeza**

Ni viunganishi ambavyo huonyesha kutolewa kwa taarifa za ziada.

Mifano ya viunganishi hivi ni zaidi ya, fauka ya, juu ya, vilevile, aidha, isitoshe na tena.

**Mifano katika sentensi**

Yeye ni mchezaji hodari, zaidi ya hayo, yeye ni mwalimu.

Mitindo ya kutahini mada hii

**Mtindo wa kwanza**

Tunga sentensi ukitumia kiunganishi cha kinyume.

Mvua ilikosa kunyesha **lakini** mimea haikukauka.

**Mtindo wa pili**

Bainisha aina za viunganishi katika sentensi ifuatayo.

(a) Walinunua sukari, majani chai na chumvi.

na kiunganishi cha kuongeza

(b) Alinunua daftari au kalamu?

au kiunganishi cha uteuzi

**Swali la KCSE 2017**

Unganisha sentensi zifuatazo kwa viunganishi mwafaka.

(i) Kheri aliweza kutujengea hospitali.

Atajenga zahanati pia.

Kheri aliweza kutujengea hospitali, isitoshe atajenga zahana-ti.

(ii) Zumari anasomea Uanasheria. Vilevile Maki anasomea Uana-sheria.

Zumari na Maki wanasomea Uanasheria.

**Mtindo wa tatu**

Ziunganishe sentensi hizi kwa kutumia kiunganishi mwafaka.

Osore amempigia Ngungui simu.

Ngungui amempigia Osore simu.

Osore na Ngungui wamepigiana simu.

Swali la KCSE 2011

Tunga sentensi moja ukitumia kiunganishi cha kinyume.

Wananchi waliteseka lakini viongozi hawakujali.

## SENTENSI TATA

Hizi ni sentensi ambazo zina maana zaidi ya moja. Utata katika sentensi hujitokeza kwa njia zifuatazo:

**(a) Neno lililo na maana zaidi ya moja**

Zipo baadhi ya sentensi ambazo huwa na maneno ambayo yana

maana zaidi ya moja. Maneno haya ambayo yana maana zaidi ya moja huleta utata katika sentensi.

**Mfano**

Wamepata chungu.

Hii ni sentensi tata. Neno **chungu** lina maana zaidi ya moja. Kwa hivyo, sentensi iliyo hapo juu itakuwa na maana zifuatazo.

1. Wamepata kifaa cha kupikia kilichoundwa kwa udongo.
2. Wamepata aina ya mdudu.
3. Wamepata upele.

**Mfano wa pili**

Watu hao watakwenda kwao.

Maana zinazojitokeza

1. Watu hao watakwenda kwa watu wengine.
2. Watu hao watakwenda mahali wanakokumiliki.

Utata wa sentensi iliyo hapo juu unatokana na neno kwao.

**(b) Utata unaotokana na mnyambuliko wa vitenzi**

Vitenzi vinaponyambuliwa hadi katika kauli ya kutendea, vinaweza kuleta maana zaidi ya moja katika sentensi.

**Mfano**

Atampigia simu.

Maana zinazojitokeza.

1. Atawasiliana na yeye kwa kutumia simu.
2. Atafanya mawasiliano ya simu kwa niaba yake.
3. Atamwadhibu kwa sababu ya simu.

**(c) Utata unaotokana na maneno mawili yaliyounganishwa na yanayohusiana**

**Mfano**

Hawa ni watoto wa marehemu Bwana Nzovu na Bi. Makambo.

Maana zinazojitokeza.

1. Watoto wanaozungumziwa wazazi wao ambao ni Bwana Nzovu na Bi Makambo wote ni marehemu.

2. Watoto hao ni wa Bwana Nzovu ambaye ni marehemu na Bi. Makambo ambaye yuko hai.

**Swali la KCSE 2009**

Kiharusi chake kimewatia hofu.

Eleza maana mbili za sentensi hii.

(i) Ugonjwa wake umewatia hofu.

(ii) Arusi aliyofanya imewatia hofu.

**Swali la KCSE 2010**

Eleza maana mbili zinazopatikana katika sentensi:

Nenda ukaniletee mbuzi.

(i) Nenda ukaniletee aina ya mnyama anayefugwa nyumbani.

(ii) Nenda ukaniltee kifaa cha kukunia nazi.

## VIREJESHI

Virejeshi ni kipashio cha lugha ambacho hurejelea nomino au kiwakilishi kinachofahamika kwa ajili ya kusisitiza. Kuna virejeshi vya aina mbili; 'o' rejeshi na kirejeshi 'amba'.

**'O' rejeshi**

Ni kiambishi ambacho hupachikwa katika vitenzi ili kurejelea nomino au kiwakilishi kinachofahamika. Kuna 'o' rejeshi kati na 'o' rejeshi tamati. **Mifano katika sentensi**

Kitabu kili**cho**potea ni chake.

Mtoto ali**ye**adhibiwa ni yule.

Virejeshi vinavyotumiwa hutegemea ngeli.

Jani lili**lo**anguka limekauka.

Mifano iliyojadiliwa hapa juu ni ya ‘o’ rejeshi kati. Hii ni kwa sababu kirejeshi kinawekwa katikati mwa kitenzi.

**Mifano zaidi**

Uzi uli**o**potea umepatikana.

Manukato yali**yo**tumiwa ni ghali.

‘O’ rejeshi tamati hupachikwa mwishoni mwa kitenzi. ‘O’ rejeshi tamati hutumiwa kuonyesha hali ya mazoea.

**Mifano katika sentensi**

Kitabu kipotea**cho** ni chake.

Mtoto aadhibiwa**ye** ni yule.

Jani liangukа**lo** hunyauka.

Virejeshi vinavyotumiwa hutegemea ngeli inayohusika.

**Mfano katika ngeli ya YA – YA**

Manukato yatumiwa**yo** ni ghali.

**Kirejeshi amba-**

Kirejeshi amba- hurejelea nomino iliyotajwa ili kusisitiza. Viambishi ambavyo hupachikwa kwenye mzizi wa kirejeshi hiki hutegemea ngeli.

**Mifano katika sentensi**

Mti **ambao** umekauka utakatwa.

Madaftari **ambayo** yamechakaa yatachomwa.

Kikapu **ambacho** kina matunda ni cha Asumini.

Kucheza ambako ni hatari kulimponza .

Virejeshi ‘o’ na ‘amba’ haviwezi vikatumiwa pamoja katika sentensi. Sentensi ifuatayo ina kasoro.

*Vitunguu ambavyo vilivyonunuliwa vitatumiwa na mpishi.

Sentensi hii inaweza ikasahihishwa kwa njia zifuatazo:

1. Vitunguu ambavyo vilinunuliwa vitatumiwa na mpishi.
2. Vitunguu vilivyonunuliwa vitatumiwa na mpishi.

**Swali**

Andika upya sentensi zifuatazo ukitumia kirejeshi **amba-.**

**(i) Kijiti kilichovunjika kilimuumiza Amina mguu.**

Kijiti ambacho kilivunjika kilimuumiza Amina mguu.

**(ii) Barua zitakazoandikwa na baba kesho zitatumwa mwaka ujao.**

Barua ambazo zitaandikwa na baba kesho zitatumiwa mwaka ujao.

**Mitindo ya kutahini mada hii,**

**Mtindo wa kwanza**

**Swali la KCSE 2011**

Tumia kirejeshi 'o' katika sentensi ifuatayo:

**Mtu ambaye hutupa tope hujichafua mwenyewe.**

Mtu atupaye tope hujichafua mwenyewe.

**Mtindo wa pili**

**Swali la KCSE 2008**

Tumia kirejeshi –amba kuunganisha sentensi zifuatazo:

(i) Mwanafunzi yule ni mrefu.

(ii) Mwanafunzi yule amepita mtihani.

Mwanafunzi yule ambaye ni mrefu amepita mtihani.

## MATUMIZI YA VIAMBISHI MBALIMBALI

**Kiambishi ki**

**(i) Hutumiwa kuonyesha udogo**.

**Mifano**

mtoto **ki**toto

mbuzi **ki**buzi

**(ii) Kiambishi hiki hutumiwa kuonyesha masharti**.

U**ki**jitahidi utafaulu.

Katika sentensi hii, kufanikiwa kwa kitendo kimoja hutegemea kitendo kingine.

U**ki**palilia mimea itanawiri.

**(iii) Kiambishi ki vilevile hutumiwa kama kipatanishi cha ngeli ya KI – VI.**

**Mifano**

Cheti chake **ki**mepatikana.

Kisu **ki**lichokuwa kikali **ki**limkata.

**(iv) Hutumiwa kuonyesha kwamba kitendo kilikuwa kikiendelea wakati kitendo kingine kilipotendeka**.

Alikuwa a**ki**lima wakati wageni walipowasili.

Sherehe zilikuwa zi**ki**endelea wakati waziri alipowasili.

(**v) Huonyesha kwamba kitendo kimekuwa kikiendelea kwa muda**.

Amekuwa a**ki**tazama filamu tangu jana.

**(vi) Kiambishi ki hutumiwa katika maneno ya lugha.**

**Mifano,** Kimeru, Kikikuyu na Kifaransa**.**

**Kiambishi ji**

**(i) Hurejelea mtendaji au watendaji**.

Huonyesha kwamba mtu au watu wamejifanyia vitendo fulani.

Wazee wame**ji**twika jukumu la kutoa ushauri kwa vijana.

Daktari ana**ji**tibu.

**(ii) Huonyesha ukubwa**.

mtu – jitu

mto – jitoto

Jito limefurika maji.

Jimeza limetengenezwa.

**(iii) Kiambishi ji hutumiwa kuonyesha mtu aliye na ujuzi wa jambo kwa muda mrefu au hali ya kuwa na mazoea.**

**Mifano**

Mchekesha**ji** amepata tuzo nyingi.

Mchezesha**ji** alitoa uamuzi sahihi katika mechi ile.

**Kiambishi li**

**(i) Hutumiwa kuonyesha wakati uliopita**.

**Mifano katika sentensi**

A**li**wasili jana.

Lango li**li**funguliwa jana asubuhi.

**(ii) Kiambishi li hutumika kama kiambishi kipatanishi cha ngeli ya LI – YA katika umoj**a.

**Mifano katika sentensi**

Tawi la mti huo **li**likatika.

Jino lake **li**ling'olewa.

**(iii) Kiambishi li hutumiwa katika kunyambua vitenzi katika kauli ya kutendea**.

**Mifano**

| **kutenda** | **kutendea** |
|---|---|
| lia | li**li**a |
| kimbia | kimbi**li**a |

Walipomwona mjomba, walimkimbilia.

**Kiambishi ku**

**(i) Hutumiwa katika kukanusha wakati uliopita**.

**Mifano**

Wanafunzi walisoma.

Wanafunzi hawa**ku**soma.

Gari liliondoka.

Gari halikuondoka.

**(ii) Huongezwa kwenye vitenzi ili kuunda nomino za vitenzi jina.**

**Mifano,** ku + cheza – kucheza

ku + lima – kulima

Kucheza kwake kunavutia.

Kulima huko kumemletea faida.

**(iii) Ni kipatanishi cha ngeli ya ku.**

Kuimba kwake **ku**napendeza.

Kuruka kwake **ku**nashangaza.

**(iv) Huonyesha nafsi ya pili umoja**.

Wazazi wata**ku**tembelea.

Abu ata**ku**nunulia ndizi.

**Kiambishi ni**

**(i) Huongezwa kwenye nomino ili kuunda vielezi**.

**Mifano**

| | |
|---|---|
| uwanja | uwanja**ni** |
| nyumba | nyumba**ni** |
| moyo | moyo**ni** |

Musa ana maumivu moyoni.

Panya ameingia shimoni.

**(ii) Huonyesha nafsi ya kwanza umoja**.

**Ni**liwaona wahalifu hao.

**Ni**tawapikia wageni wote.

**(iii) Huongezwa mwishoni mwa vitenzi ili kuonyesha wingi au amri**.

**Mifano**

cheze**ni**

imbe**ni**

ruke**ni**

**(iv) Hutumiwa kubainisha mtendwa.**

Ali**ni**zawidi kwa kazi niliyoifanya.

**Kiambishi ka**

**(i) Hutumika katika hali ambapo amri inatolewa**.

**Mifano**

**Ka**cheze!

**Ka**lime!

**(ii) Hutumiwa kuonyesha wakati usiodhihirika**.

Mwalimu a**ka**mtuma achukue daftari lake.

**(iii) Kiambishi ka huonyesha mfuatano wa vitendo**.

Wanariadha walikimbia, wa**ka**nyosha viungo, wa**ka**fanya mkutano kisha wa**ka**ondoka.

**(iv) Hutumika kama kiishio katika mnyambuliko wa vitenzi katika kauli ya kutendeka**.

Taa ilizimi**ka** mlango ulipofunguliwa .

Chakula hakikuli**ka** kwani hakikuwa na chumvi.

**Matumizi ya kwa**

**(i) Huonyesha kifaa kilichotumiwa kufanyia kazi fulani.**

Alikata kitambaa kwa makasi.

Walisafiri kwa meli.

**(ii) Hubainisha akisami**.

Alizoa alama tisa kwa kumi katika jaribio hilo.

**(iii) Kwa ni kiambishi kinacholeta dhana ya pamoja na.**

Wazee kwa vijana walishirikiana katika mradi huo.

Wanasiasa kwa wananchi walijitolea kuleta maendeleo katika nchi.

**(iv) Hudhihirisha namna kitendo kilivyofanyika**.

Msichana mrembo alitembea kwa maringo.

Kiongozi fisadi alisema kwa ujeuri.

**(v) Kiambishi kwa hutumiwa kuonyesha sababu ya kufanyika kwa kitendo fulani**.

Waliadhibiwa kwa kuchelewa kufika shuleni.

**(vi) Huonyesha mahali.**

Watoto wamekwenda kwa wazazi wao.

**(vii) Katika baadhi ya misemo, kwa hutumiwa**.

**Mifano,** ana kwa ana

uso kwa macho

**(viii) Huonyesha muda**.

Walifanya mtihani huo kwa saa tatu.

**(ix) Hudhihirisha njia zilizotumiwa ili kufikia hali fulani**.

Walifika mjini kwa kutembea.

**Matumizi ya na**

(i) **Huonyesha wakati uliopo**.

Waziri a**na**soma hotuba yake.

**(ii) Hutumika kama kiunganishi**.

Ng'ombe **na** mbuzi wamepelekwa malishoni.

**(iii) Hutumika kama kiishio katika mnyambuliko wa vitenzi kauli ya kutendana au kutendeana**.

Watoto wanarushia**na** mpira.

**(iv) Hudhihirisha mtendaji wa jambo**.

Hotuba ilitolewa **na** Rais.

Mgomo uliongozwa **na** mwenyekiti.

**Matumizi ya 'po'**

**(i) Hudhihirisha wakati**.

Ali**po**ingia, wananchi walisimama.

Kengele ili**po**pigwa, wanafunzi walitoka darasani.

**(ii) Kiambishi 'po' hutumiwa kuonyesha mahali**.

Wana**po**chezea pana mchanga tele.

Kuna mitindo miwili inayotumiwa kutahini mada hii.

**Mtindo wa kwanza**

Kueleza matumizi ya viambishi mbalimbali.

**Mfano**

Eleza matumizi mawili ya kiambishi ni.

**Mtindo wa pili**

Kubainisha matumizi ya kiambishi fulani kilichotumiwa katika sentensi.

**Mfano**

Ainisha matumizi ya kiambishi ki katika sentensi ifuatayo.

<u>**Ki**</u>toto hiki <u>**ki**</u>napenda uji.

udogo kiambishi cha ngeli

**Swali la KCSE 2016**

Eleza matumizi mawili ya kiambishi –ji-.

(i) Huonyesha ukubwa wa nomino.

mto – jito

(ii) Hurejelea mtendaji.

Yeye ali**ji**katia keki.

**Swali la KCSE 2017**

Tumia kwa katika sentensi kuonyesha:

(i) Sehemu ya kitu kizima.

Mwanafunzi hodari alipata arobaini kwa hamsini katika jaribio hilo.

(ii) Namna tendo lilivyofanyika.

Alitembea kwa maringo alipokwenda kuchukua zawadi.

## A UNGANIFU

'A' unganifu hutumika katika miktadha ambapo kuna uhusiano wa vipashio viwili vya lugha. Hutegemea ngeli inayohusika. 'A' unganifu inaweza kutumika kama kivumishi, kiwakilishi au kihusishi.

**Mifano**

**La** mkulima limevunjika.

**kiwakilishi**

Katika sentensi hii 'a' unganifu inaleta dhana ya kumiliki.

**Wa** kwanza ametuzwa zawadi.

**kiwakilishi** (kinaonyesha mahali katika foleni au nafasi katika kundi)

Kisu **cha** chuma hudumu.

**kivumishi** cha 'a' unganifu

Unga **wa** mahindi umetumiwa na mpishi.

**kivumishi** cha 'a' unganifu (kuonyesha aina)

**Swali la KCSE 2013**

Tumia kiwakilishi cha 'a' unganifu katika sentensi kuonyesha:

(i) umilikaji

(ii) nafasi katika orodha au nafasi katika kundi

**Cha** mhunzi kimepotea.

Kiwakilishi cha 'a' unganifu kinachoonyesha umilikaji.

**Wa** pili atapewa shilingi elfu kumi.

Kiwakilishi cha 'a' unganifu kinachoonyesha nafasi katika orodha au nafasi katika kundi.

Mitindo ya kutahini mada ya 'a' unganifu.

**Mtindo wa kwanza**

Tumia kiwakilishi cha 'a' unganifu katika sentensi kuonyesha:

(a) aina

(b) nafasi katika orodha

(c) umilikaji

**Cha** chuma kinadumu.

Kiwakilishi kinachoonyesha aina.

**Wa** kwanza atapewa madini ya dhahabu.

nafasi katika orodha

**Ya** wakulima yametumiwa.

umilikaji

Jedwali lifuatalo linaonyesha 'a' unganifu kwa kutegemea ngeli.

| NGELI | UMOJA | WINGI |
|---|---|---|
| A –WA | wa | wa |
| U – I | wa | ya |
| KI – VI | cha | vya |
| LI – YA | la | ya |
| U – ZI | wa | za |
| I – ZI | ya | za |
| YA – YA | ya | ya |
| I – I | ya | ya |
| U – U | wa | wa |
| U – YA | wa | ya |
| PA | pa | pa |
| KU | kwa | kwa |
| MU | mwa | mwa |

## UCHANGANUZI WA SENTENSI

Kuna njia tatu zinazotumika katika uchanganuzi wa sentensi. Njia hizo ni:

**(a) michoro ya matawi**

**(b) majedwali**

**(c) mishale au mistari**

Uchanganuzi wa sentensi huanza kwa kuonyesha sentensi (S).

Baada ya hatua hii, kikundi nomino (KN) na kikundi tenzi (KT) hufuatia.

Kisha maneno yanayopatikana katika kikundi nomino na kikundi

tenzi hudhihirishwa. Herufi mbalimbali hutumiwa kuonyesha maneno tofautitofauti. Ni lazima herufi hizi ziwe kubwa .

kitenzi kikuu au halisi **T**

kitenzi kisaidizi **Ts**

kiwakilishi **W**

kihisishi **I**

kielezi **E**

nomino **N**

kiunganishi **U**

kivumishi **V**

kihusishi **H**

**Mifano**

1 Changanua sentensi ifuatayo kwa kutumia mishale.

Mito imechafuka sana.

S → KN + KT

KN → N

N → Mito


KT → T + E

T → imechafuka

E → sana.

2 Chora vielelezo matawi vya sentensi ifuatayo.

Baba na kaka wanacheza mpira.



3 Changanua sentensi hii kwa kutumia jedw

Waliwatembelea wazee hao.

| S | | | |
|---|---|---|---|
| KN | KT | | |
| N | T | KN | |
| | | N | V |
| Ө | Waliwatembelea | wazee | hao. |

4 Changanua sentensi ifuatayo kwa kutumia mistari.

Zippy, Mary na Mumbi wanapenda maziwa.

S —— KN + KT

KN —— N + N + U + N

N —— Zippy

N —— Mary

U —— na

N —— Mumbi

KT —— T + KN


T —— wanapenda

KN —— N

N —— maziwa.

5. Ichoree sentensi ifuatayo matawi.

Maziwa yalimwagika walipokuwa wanacheza.




6. Changanua sentensi ifuatayo kwa kutumia jedwali.

Mkimbizi anaishi kambini kwa kuwa aliteseka porini.

| S | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| $S_1$ | | | U | $S_2$ | | |
| KN | KT | | | KN | KT | |
| N | T | E | | N | T | E |
| Mkimbizi | anaishi | kambini | kwa kuwa | Ɵ | aliteseka | porini. |

7. Changanua sentensi ifuatayo kwa kutumia mishale.


Wazee wanafanya mazungumzo ilhali vijana wanalima shambani.

S → S1 + U + S2
S1 → KN + KT
KN → N
N → Wazee
KT → T + KN
T → wanafanya
KN → N
N → mazungumzo

U → ilhali
S2 → KN + KT
KN → N
N → vijana
KT → T + E
T → wanalima
E → shambani.

8 Ichoree vielelezo matawi sentensi:

Shamba hili lililokuwa na migogoro limeuzwa.




9 Changanua sentensi ifuatayo ukitumia mistari.

Maria alipika taratibu huku mama akimwelekeza vizuri.

S ———— S1 + U + S2

| | | | |
|---|---|---|---|
| S1 ———— | KN + KT | S2 ———— | KN + KT |
| KN ———— | N | KN ———— | N |
| N ———— | Maria | N ———— | mama |
| KT ———— | T + E | KT ———— | T + E |
| T ———— | alipika | T ———— | akimwelekeza |
| E ———— | taratibu | E ———— | vizuri. |
| U ———— | huku | | |


10. Changanua sentensi ifuatayo kwa kutumia jedwali.

Chakula ambacho kilipikwa kiliiva vizuri sana.

<table>
<tr><td colspan="5">S</td></tr>
<tr><td colspan="2">KN</td><td colspan="3">KT</td></tr>
<tr><td>N</td><td>S</td><td>T</td><td colspan="2">KE</td></tr>
<tr><td rowspan="2">Chakula</td><td rowspan="2">ambacho kilipikwa</td><td rowspan="2">kiliiva</td><td>E</td><td></td></tr>
<tr><td>vizuri</td><td>sana.</td></tr>
</table>

11. Ichoree vielelezo vya matawi sentensi ifuatayo,

Hili lake lilikuwa limeiva lakini hatukujua.




12. Changanua sentensi ifuatayo kwa kutumia jedwali.

Mbuzi hao wanakula nyasi malishoni.

| S | | | | |
|---|---|---|---|---|
| KN | | KT | | |
| N | V | T | KN | |
| | | | N | E |
| Mbuzi | hao | wanakula | nyasi | malishoni. |

13. Changanua sentensi ifuatayo kwa njia ya mishale.

Kile kifupi kimemkata vibaya sana.

S → KN + KT

KN → W + V

W → kile

V → kifupi

KT → T + KE

T → kimemkata


KE → E + E2

E → vibaya

E2 → sana

14. Ichoree vielelezo vya matawi sentensi.

Tunda limechumwa hata ingawa halijaiva.




15. Changanua sentensi hii kwa kutumia jedwali.

Daftari lililosahihishwa na mwalimu lilianguka majini jana asubuhi.

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| S | | | | | |
| KN | | KT | | | |
| N | S | T | KE | | |
| | | | E | E | E |
| Daftari | lililosahihishwa | lilianguka | majini | jana | asubuhi. |

16. Changanua sentensi ifuatayo kwa kutumia mistari.

Ukuta ulibomoka walipokuwa wakiuparaga.

S ——— KN + KT

KN ——— N

N ——— Ukuta


KT ——— T + S

T ——— ulibomoka

S ——— walipokuwa wakiuparaga.

17. Ichoree vielelezo vya matawi sentensi ifuatayo.

Mkutano huo ulifanyika mbele ya jukwaa.




18. Changanua sentensi hii kwa kutumia jedwali.

Gari hilo lilikuwa limeharibika, hata hivyo halikupelekwa gereji.

| S | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| S1 | | | | U | S2 | | |
| KN | | KT | | | KN | KT | |
| N | V | Ts | | | N | T | KN |
| | | | | | | | N |
| Gari | hilo | lilikuwa | limeharibika | hata hivyo | Θ | halikupekwa | gereji. |

19 Changanua sentensi hii kwa kutumia mishale.

Lo! Kijana yule amemtusi babake.

S → KN + KT

KN → I + N + V

I → Lo

N → Kijana

V → yule

KT → T + KN


T → amemtusi

KN → N

N → babake.

20. Chora vielelezo matawi vya sentensi ifuatayo:

Mwanamuziki hodari amepokea tuzo nyingi.



## USEMI HALISI NA USEMI WA TAARIFA

## USEMI HALISI

Haya ni maneno halisi yaliyosemwa na msemaji bila ya kuyabadilisha. Maneno haya huandikwa jinsi msemaji alivyoyatamka.

**Mifano**

“Nitakuja kesho,” mama alisema.

Waziri wa Afya alisema, “Ugonjwa huu ni hatari sana.”

Katika usemi halisi, mambo yafuatayo huzingatiwa:

**(a) Alama za mtajo hutumiwa**.

**Mfano,** “Nitakununulia zawadi,” mama alimwahidi mwanawe.

Dereva alisema, “Mjifunge mikanda ya usalama.”

**(b) Herufi kubwa hutumiwa mwanzoni mwa kauli ya msemaji**.

“Machungwa haya ni matamu,” mshitiri alisema.

**(c) Alama zote za uakifishaji huwekwa ndani ya alama za usemi**.

“Njoo hapa haraka!” Askari alimwamrisha mfungwa.

“Utakunywa chai au uji?” Mjomba aliniuliza.

**(d) Endapo wasemaji ni wawili kauli zao haziwekwi pamoja bali hutenganishwa**.

Mzee alimwambia mwanawe, “Njoo nikupeleke kwa babu yako angalau umjue.”

Mtoto aliuliza, “Nani babu?”

**(e) Ikiwa kauli ya msemaji inaendelea, herufi ndogo itatumiwa katika sehemu ya pili ya kauli ya msemaji.**

“Tunafaa kuyahifadhi mazingira, ” Waziri wa Mazingira alisema, “yanatusaidia ili tupate mvua.”

**(f) Maneno yanayonukuliwa yakitokea mwishoni, alama ya koma hutumiwa kabla ya alama za kunukuu**.

Opiyo alisema, “Wazazi wangu watasafiri kesho.”

**(g) Maneno yanayonukuliwa yanapotangulia, aghalabu alama ya koma hutumika kabla ya alama za usemi za kufungia**.

“Shule yetu ina wanafunzi wengi,” mwanafunzi alisema.

**(h) Endapo kauli ya msemaji inaendelea na ikiwa sehemu ya kwanza ya kauli yake imekamilika, sehemu ya pili ya kauli yake itaanza kwa herufi kubwa**.

“Shughuli zangu zote zimekamilika.” Magoka akasema, “Nitakuwa ninawapokea wageni mwezi ujao.”

## USEMI WA TAARIFA

Ni maelezo ya yale yaliyosemwa na msemaji. Katika usemi wa taarifa mambo yafuatayo huzingatiwa:

**(i) Alama za kunukuu hazitumiwi.**

usemi halisi “Nitakuja kesho,” mama alisema.

usemi wa taarifa Mama alisema kwamba angekuja siku ambayo ingefuata.

**(ii) Neno kwamba au kuwa linaweza likatumika katika usemi wa taarifa**.

**(iii) Alama ya kuuliza au hisi haitumiki**.

“Umeuza viti vingapi?” Baba aliniuliza.

Baba alitaka kujua nilikuwa nimeuza viti vingapi.

**(iv) Maneno mbalimbali huweza kubadilika**.

**Mifano ya maneno hayo ni**

| **usemi halisi** | **usemi wa taarifa** |
|---|---|
| kesho | siku ambayo ingefuata |
| leo | siku hiyo |
| mwaka jana | mwaka uliotangulia |
| jana | siku iliyotangulia |
| hapa | hapo |
| aliuliza | alitaka kujua |

| | |
|---|---|
| wangu | wake |
| huyo | yule |
| sasa | wakati huo |
| kwa nini | alitaka kujua |
| yetu | yao |
| chenu | chao |

**(v) Aghalabu wakati uliopita hutumika.**

"Mzigo huu ni wangu," hamali alilalamika.

Mjomba alisema kuwa mzigo huo ulikuwa wake.

**Swali la KCSE 2016**

"Shughuli yetu itakamilika kesho," mama alimwambia mwanawe Juma. (Andika katika usemi wa taarifa)

Mama alimwambia mwanawe Juma kwamba shughuli yao ingekamilika siku ambayo ingefuata.

**Swali la KCSE 2017**

Andika sentensi ifuatayo katika usemi wa taarifa.

"Kusoma kwa mapema kutapalilia ubunifu wa wanafunzi hawa wenu," mtaalamu akatuambia.

Mtaalamu alitwambia kwamba kusoma kwa mapana kungepalilia ubunifu wa wanafunzi hao wetu.

**Swali la KCSE 2006**

Andika katika msemo wa taarifa.

"Sitathubutu kumpa pesa zangu." Mkolwe alisema.

Mkolwe alisema kuwa hangethubutu kumpa pesa zake.

**Swali la KCSE 2009**

Andika kwa msemo halisi.

Baba alipotuuliza kama tungependa kwenda Mombasa wakati wa likizo tulimjibu kwamba tulitaka kwenda Kisumu kwa kuwa tulikuwa hatujaliona Ziwa Victoria.

“Mtapenda kwenda Mombasa wakati wa likizo?” Baba alituuliza.

“Tunakata kwenda Kisumu kwani hatujaliona Ziwa Victoria.” Tulimjibu.

Mitindo ya kutahini mada hii,

(a) Andika sentensi ifuatayo katika sentensi usemi wa taarifa.

**“Mchezo wa miguu utaanza sasa,” mchezaji akasema.**

Usemi wa taarifa. Mchezaji alisema kwamba mchezo wa miguu ungeanza wakati huo.

(b) Andika sentensi ifuatayo katika usemi halisi.

**Kiongozi alisema kuwa taifa lao lingepiga hatua ikiwa wangewajibika**.

“Taifa letu litapiga hatua ikiwa tutawajibika,” kiongozi alisema.

(c) Akifisha sentensi ifuatayo.

**nitawaletea matunda mengi solemba alisema ili yatumike katika biashara yenu**.

“Nitawaletea matunda mengi,” Solemba alisema, “ili yatumi-ke katika biashara yenu.”

## VIAMBISHI NA MOFIMU

Viambishi ni silabi ambazo huongezwa kwenye mizizi ya maneno ili kuleta maana katika maneno yenyewe. Viambishi hivi vinaweza kuwekwa kabla au baada ya mzizi wa neno. Viambishi ambavyo huwekwa kabla ya mzizi wa neno hufahamika kama viambishi awali. Viambishi ambavyo huwekwa baada ya mzizi wa neno hujulikana kama viambishi tamati.

**Viambishi awali**

Hivi ni viambishi ambavyo huwekwa kabla ya mzizi wa neno.

**Aina za viambishi awali**

(a**) Kiambishi awali cha nafsi**

Hivi ni viambishi ambavyo huonyesha nafsi mbalimbali.

| Nafsi | Umoja | Wingi |
|---|---|---|
| ya kwanza | ni - | tu- |
| ya pili | u- | m- |
| ya tatu | a- | wa- |

**Ni**tawapikia wageni.

**Wa**likuja jana.

**M**tafanya kazi hiyo.

**(b) Kiambishi awali cha ngeli**

Huwakilisha ngeli mbalimbali.

**A**nacheza uwanjani.

Ngeli ya A – WA

**ki**lichovunjika

kiambishi awali cha ngeli ya KI - VI

**u**liokatwa

kiambishi awali cha ngeli ya U – I

**(c) Kiambishi awali cha nyakati au hali**

tu**li**panda

kiambishi awali cha wakati uliopita

a**me**shuka

kiambishi awali cha hali timilifu

**(d) Kiambishi awali kirejeshi**

tuli**lo**lipiga

kiambishi awali kirejeshi

ana**ye**cheza

kiambishi awali kirejeshi

**(e) Kiambishi awali cha mtendwa**

uliye**m**kuta

kiambishi awali cha mtendwa

aliye**ni**fundisha

kiambishi awali cha mtendwa

**(f) Kiambishi awali cha mtendaji**

ame**ji**kata

kiambishi awali cha mtendaji

**(g)** Kiambishi **awali cha kukanusha**

**si**takuja

kiambishi awali cha kukanusha

**Viambishi tamati**

Hivi ni viambishi ambavyo huwekwa baada ya mzizi wa neno.

**Aina za viambishi tamati**

**(a) Viambishi tamati vya mnyambuliko**.

zilikat**w**a

kiambishi tamati cha mnyambuliko

chez**esh**a

kiambishi tamati cha mnyambuliko

**(b) Kiambishi tamati kiishio**

limi**a**

Kiambishi tamati kiishio au **kiambishi tamati cha kauli ya kutenda**.

andiki**a**

kiambishi tamati kiishio

**(c) Kiambishi tamati kirejeshi**

wacheza**po**

kiambishi tamati kirejeshi

waingia**mo**

kiambishi tamati kirejeshi

(d) **Kiambishi tamati cha wingi/ amri**

Ruke**ni**

## MOFIMU

Mofimu hurejelea sehemu ndogo sana katika neno na ambayo huwasilisha maana.

**Mifano**

**ulicheka**

u- mofimu ya nafsi

li- mofimu ya wakati

chek- mofimu ambayo ni mzizi wa kitenzi

a-mofimu kiishio

**watoto**

wa- mofimu ya wingi

toto- mofimu ambayo ni mzizi

**Aina za mofimu**

**Mofimu huru**

Ni mofimu ambazo hujisimamia kimaana. Mofimu hizi hazitegemei mofimu nyingine ili kuwasilisha maana. Mifano mofimu huru ni:

chumvi simu umio hodari

chai gitaa maji sugu

kaka saa kamusi haraka

mimi

Baadhi ya maneno ambayo ni mofimu huru ni kama vivumishi, baadhi ya nomino, vielezi na viwakilishi.

**Mofimu tegemezi/Mofimu ambata**

Hizi ni mofimu ambazo haziwezi kuwasilisha maana zikiwa peke yake. Mofimu hizi huhitaji mofimu nyingine ili kuwasilisha maana. Mifano ya mofimu hizi ni baadhi ya nomino, vitenzi na mizizi ya maneno mengine.

**Mifano**

anacheza, mtoto na watu

**anacheza**

a-mofimu ya nafsi

na- mofimu ya wakati

chez- mofimu ambayo ni mzizi

a-mofimu kiishio

**mtoto**

m- mofimu ya umoja

toto- mofimu ambayo ni mzizi

**watu**

wa- mofimu ya wingi

tu- mofimu mzizi

Mitindo ya kutahini mada hii:

1. Ainisha aina za mofimu katika maneno yafuatayo.

(i) gesi

(ii) kitabu

gesi mofimu huru

kitabu mofimu tegemezi

2. Bainisha mofimu katika neno,

walizokimbiza

wa- mofimu ya nafsi

li- mofimu ya wakati

zo- mofimu kirejeshi

kimbiz- mofimu ya mzizi

a-mofimu kiishio

3 Andika neno lenye muundo ufuatao,

(i) kiambishi cha ngeli, wakati uliopo, kirejeshi, mzizi, kauli tendwa, kauli tenda

linalopigwa

(ii) kiambishi cha umoja, mzizi

mkulima

**Swali la KCSE 2016**

Tambua kiambishi awali na tamati katika neno:

alalaye

a-kiambishi awali cha nafsi ye- kiambishi tamati kirejeshi

Ainisha mofimu katika maneno yafuatayo:

(i) asemavyo

a-mofimu ya nafsi

sem- mofimu mzizi

a-mofimu ya kauli ya kutenda

vyo-mofimu kirejeshi

(ii) mwangwi

mw- mofimu ya umoja

angwi- mofimu ya mzizi

**Swali la KCSE 2013**

Bainisha mofimu katika neno:

**atamnywea**

a-mofimu ya nafsi

ta- mofimu ya wakati

m- mofimu ya mtendwa

nyw- mofimu ya mzizi

a-kiishio

## MNYAMBULIKO WA VITENZI

Kunyambua vitenzi ni kuongeza viambishi kwenye mizizi ya vitenzi ili kuleta maana tofauti. Vitenzi katika lugha ya Kiswahili vinaweza vikanyambuliwa katika kauli mbalimbali.

Mnyambuliko wa vitenzi vya silabi.

Mifano ya vitenzi vya silabi moja ni ja, fa, nya, wa, pa, nywa na la.

| | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| kutenda | fa | ja | nya | wa | pa | nywa | la | chwa |
| kutendea | fia | jia | nyea | wia | pea | nywia | lia | chwea |
| kutendwa | - | - | - | - | pewa | - | - | - |
| kutendeana | - | - | - | wiana | peana | - | liana | - |
| kutendewa | - | jiwa | nyewa | wiwa | - | nywewa | liwa | - |
| kutendeka | - | jika | nyeka | - | - | nyweka | lika | - |
| kutendesha | fisha | jisha | nyesha | - | | nywesha | lisha | |

**Mifano katika sentensi**

Mbwa **alifia** mtoni.

Watoto **waliliana** chakula.

Kinywaji hicho kikali **kilinyweka.**

Mnyambuliko wa vitenzi vingine

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| kutenda | piga | choma | kosesha | cheka | eleza | dhamini |
| kutendea | pigia | chomea | koseshea | chekea | elezea | dhaminia |
| kutendwa | pigwa | chomwa | koseshwa | chekwa | elezwa | - |
| kutendewa | pigiwa | chomewa | koseshewa | chekewa | elezewa | dhaminiwa |
| kutendeka | pigika | chomeka | kosesheka | chekeka | elezeka | dhaminika |
| kutendesha | - | chomesha | - | chekesha | elezesha | dhaminisha |
| kutendana | pigana | chomana | koseshana | chekana | elezana | - |
| kutendeana | pigiana | chomeana | kosesheana | chekeana | elezeana | dhaminiana |

Vitenzi vya asili ya Kibantu huishia kwa irabu a. Mfano ni kama lima, cheza, pika, ruka na panga.

Vitenzi vyenye asili ya kigeni huishia kwa irabu, e, u, i na o. Mifano ya vitenzi hivi ni dhamini, laki, husu, tibu na rudufu.

Katika kuvinyambua vitenzi, mwanafunzi anahitajika kuangalia kiishio cha kauli anayohitajika kunyambua. Kitenzi anachonyambua kinafaa kuwa na kiishio sawa na kiishio cha kauli anayohitajika kuinyambua.

**Mfano wa kwanza**

**Nyambua kitenzi jaliza katika kauli ya kutendeana/kufanyi-ana**.

Viishio vya kauli inayohusika ni **–eana/iana**. Ina maana kwamba kitenzi jaliza kitaishia kwa **–iana** au –**eana**. Kwa kuwa kwenye mzizi wa kitenzi hiki kuna irabu **i**, kitakaponyambuliwa kitaishia kwa **–iana**.

| **kutenda** | **kutendeana** |
|---|---|
| jaliza | jaliziana |

**Mfano wa pili**

**Kinyambue kitenzi chora katika kauli ya kutendesha**.

Kiishio cha kauli ya mnyambuliko huu ni **–esha**. Kwa kuwa kitenzi chenyewe kina irabu **o** kwenye mzizi, kitenzi chora kwa hivyo ni **choresha** katika kauli ya kutendesha.

Katika mnyambuliko wa vitenzi, mizizi ya vitenzi ambayo ina irabu **a**, **e**, **i** na **u** huchukua irabu **i** katika mnyambuliko.

**Mfano**

| **kutenda** | **kutendea** |
|---|---|
| piga | pigia |
| kata | katia |
| keti | ketia |
| kubali | kubalia |

Mizizi ya vitenzi iliyo na irabu **o** na **u** huchukua irabu **e** katika mnya-mbuliko wa vitenzi.

**Mifano**

| **kutenda** | **kutendea** |
|---|---|
| chora | chorea |
| soma | somea |
| bopa | bopea |

Mitindo ya kutahini mada ya mnyambuliko wa vitenzi.

1. Jaliza jedwali lifuatalo.

| Kutenda | Kutendesha |
|---|---|
| iga | |
| | kubalisha |

iga - igiza

kubali – kubalisha

2. Geuza sentensi ifuatayo iwe katika kauli ya kutendea.

Alipiga simu.

Alimpigia simu.

3. Nyambua vitenzi vifuatavyo viwe katika kauli zilizo kwenye mabano.

(i) ja (kutendesha) jisha

(ii) vaa (kutendwa)valiwa

(iii) nya (kutendeka) nyeka

(iv) wa (kutendewa) wiwa

## UUNDAJI WA MANENO

Kuna njia mbalimbali zinazotumiwa katika kuunda maneno. Uundaji wa maneno ni kuibuka na maneno mapya katika lugha ya Kiswahili.

### 1. Kuunda nomino kutoka kwa vitenzi

Zipo baadhi ya nomino ambazo huundwa kutokana na vitenzi.

**Mifano**

| **kitenzi** | **nomino** |
|---|---|
| cheka | kicheko, cheko |
| piga | pigo, kipigo |
| cheza | mchezaji, uchezaji, mchezo |
| imba | wimbo, mwimbaji, uimbaji |
| jenga | jengo, mjengo, ujenzi |
| dai | mdai, mdaiwa |
| eleza | maelezo |
| kopa | mkopo, mkopi, mkopeshaji |

jaa mjao, ujazo

Kuna baadhi ya vitenzi ambavyo ni vigumu kuunda nomino. Hata hivyo kwa kuongeza kiambishi **ku** katika vitenzi hivyo unapata **nomino ya kitenzi jina**.

**Mifano**

ku + tarazaki - kutarazaki

ku + pogoa - kupogoa

**2. Kuunda vitenzi kutoka kwa nomino**

| **nomino** | **vitenzi** |
|---|---|
| msafiri | safiri |
| mpango | panga |
| kilio | lia |
| mkao | kaa |
| ubashiri | bashiri |
| utelezi | teleza |
| uneni | nena |
| ghadhabu | ghadhibika |

Mifano ya maswali

1. Unda nomino kutokana na vitenzi vifuatavyo.

(i) dahua

(ii) kinaisha

**Majibu**

kudahua

kukinaisha

**3. Kuunda vivumishi kutoka kwa nomino**

| **nomino** | **vivumishi** |
|---|---|
| ucheshi | mcheshi |
| ukakamavu | mkakamavu |

ufisadi fisadi

ukamilifu kamili

Andika upya sentensi ifuatayo ukibadilisha vitenzi vilivyomo kuwa nomino.

Mayaka anapotumbuiza huchekesha sana.

**Kutumbuiza kwa Mayaka kuna ucheshi**.

## VINYUME VYA VITENZI

Ni hali ya kuandika vitenzi vinavyokinzana kimaana na vitenzi vilivyo-tajwa.

Hakuna kinyume cha nomino. Kinyume hudhihirika tu katika vitenzi, vivumishi na vielezi. Katika sentensi zilizo na vitenzi viwili, kinyume kitadhihirika tu katika kitenzi kimoja tu.

**Mifano katika sentensi,**

**Nataka mpira ulio na hewa.**

Sitaki mpira ulio na hewa. (kinyume)

Jawabu lifuatalo sio sahihi

***Sitaki mpira usiyo na hewa**.

Alianika nguo zote.

**Alianua** nguo zote. (kinyume)

Juma aliziba ufa huo.

Juma **alizibua** ufa huo. (kinyume)

Hakuna kinyume cha jinsia.

Mama aliinjika chungu mekoni.

Mama aliepua chungu mekoni. (kinyume)

Vinyume vya vitenzi huweza kutokea kwa kuvinyambua vitenzi au kuandika neno tofauti kabisa na lililotajwa.

**Mifano**

| **neno** | **kinyume** |
|---|---|
| ziba | zibua |

choma chomoa

fuma fumua

injika epua

chekalia

**Mifano katika sentensi**

Fundi alishuka mtini.

Fundi alipanda mtini. (kinyume)

## MIUNDO YA SENTENSI

Sentensi ya Kiswahili huwa na maneno mbalimbali. Maneno haya ni kama nomino, vivumishi, vihusishi, viunganishi, viwakilishi, vihusishi au vitenzi.

Herufi tofauti hutumika katika kubainisha maneno mbalimbali. Mifano ya herufi hizo ni:

N- nomino H- kihusishi

V - kivumishi T- kitenzi kikuu au halisi

E - kielezi Ts- kitenzi kisaidizi

I - kihisishi t- kitenzi kishirikishi

U - kiunganishi KN- kikundi nomino

W - kiwakilishi KE- kikundi elezi

KT - kikundi tenzi

RS - kirai kihusishi

Katika mada hii, mwanafunzi atatahiniwa katika njia zifuatazo:

Mtindo wa kwanza

1. Tunga sentensi zenye miundo ifuatayo:

(a) KN (N + RH) + KT (Ts + T)

(b) KN (V + N) + KT (t + V)

Majibu

(a) Mwanasiasa mbele ya jukwaa alikuwa anawahutubia.

(b) Yule mvulana ni mtundu.

Tunga sentensi yenye muundo ufuatao:

KN(N + RH) + KT (T + E)

Kitabu juu ya meza kitatumiwa shuleni.

**Mtindo wa pili**

1. Tunga sentensi yenye muundo ufuatao:

kiwakilishi, kitenzi kisaidizi, kitenzi kikuu, nomino

Yule alikuwa anacheza mpira.

kihisishi, nomino, kivumishi, kitenzi kishirikishi kipungufu, nomino

Lo! Mwanamume yule ni mwizi.

**Mtindo wa tatu**

Iandike upya sentensi ifuatayo kwa kutumia kiwakilishi badala ya nomino iliyopigwa mstari.

**Mwalimu** anafuta ubao.

**Huyu** anafuta ubao.